Jumanne Juni 15, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580612

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**Ongezeko** kina cha maji Ziwa Victoria lakwamisha ujenzi Daraja la JPM

UKURASA 2



**Mufti** ataka kesi ya viongozi wa Uamsho iharakishwe kusikilizwa

UKURASA 3

Neymar atisha Brazil ikiiua Venezuela Copa America

UKURASA 20

# Mjadala kodi za majengo moto

• **Wabunge** wataka ufafanuzi ulipaji kwa mfumo wa Luku nyumba za wapangaji... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**SERIKALI YASISITIZA UVAAJI WA BARAKOA**
WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy...

UKURASA WA 4
**RAIS SAMIA, VYAMA VYA SIASA WAMLILIA BAREGU**
RAIS Samia Suluhu Hassan, amemwelezea mwanazuoni na aliyekuwa...

UKURASA WA 7
**KAMATI YASHAURI MITAALA YA ELIMU KUPITIWA UPYA**
KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imesema licha ya ubora wa...




## Wenye namba NIDA kupata vitambulisho mwezi Agosti

UKURASA 3



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play
Download on the App Store



## Mbowe ataja 'wachawi' ndani ya CHADEMA

UKURASA 16

**MICHEZO** UCHAGUZI TFF WABURUZANA FIFA UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mjadala kodi za majengo moto

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WABUNGE wametaka serikali itoe ufafanuzi kuhusu suala la utozaji wa kodi ya majengo kwa mfumo wa Luku, kwamba atakayebeba mzigo huo ni nani kati ya mpangaji au mmiliki wa jengo.

Wakichangia bajeti ya serikali iliyowasilishwa Alhamisi iliyopita pamoja na taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Fedha iliyowasilishwa jana bungeni, wabunge walisema suala hilo lina sintofahamu kati ya wapangaji na wamiliki wa majengo.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Juliana Shonza, alisema kodi ya majengo ilikuwapo miaka mingi, lakini matatizo yake ni wananchi walikuwa hawalipi akiwamo yeye.

"Sijawahi kulipa kodi ya majengo na ni kutokana na usumbufu ambao ukifikiria utoke ukapange foleni TRA, lakini serikali imekuja na ubunifu wa kukusanya kodi hii na imetumia akili ikusanywe kwa akili kuliko kutumia mabavu," alisema.

Shonza alisema yapo matatizo yaliyopo kwenye kodi hiyo, na kwamba wanatambua serikali imekuja na jambo jema na ubunifu mzuri, lakini ni lazima isimamie ili katika utekelezaji wa agizo hilo kusiibuke sintofahamu.

"Sheria ya majengo ya awali inasema kabisa kwamba suala la kulipa kodi ya majengo ni la mwenye nyumba na siyo suala la mpangaji.

"Kwa hiyo kwenye agizo hili nimwombe sana mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, atakaposimama hapa atuambie serikali imejipangaje, ina mkakati gani ili kuondoa sintofahamu kati ya mwenye nyumba na mpangaji.

"Ni kweli mmiliki wa nyumba ni mwenye nyumba kwa kuwa kodi inakatwa kwenye Luku maana naye atakayekatwa ni mpangaji siyo mwenye nyumba, naomba serikali ije na utaratibu mzuri kuhusiana na kodi hii."

Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, alihoji kodi ya majengo ambayo inatozwa kwa njia ya Luku atakayetozwa ni mwenye jengo au mpangaji.

"Sasa hapo unamtoza mwenye jengo au mpangaji, tuangalie namna nzuri ya kukusanya mapato haya," alisema.

Mbunge wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage, alisema alisema wazo hilo lina ubunifu ndani yake na kutoa angalizo kwamba yupo mtu ana nyumba ya ghorofa kwa maana vyumba viwili juu na viwili chini na analipa Sh. 5,000 na kuhoji mwenye vyumba vitano chini kwa nini alipishwe Sh. 1,000.

"Kuna mtu ana vyumba saba ana wapangaji watatu na kila mmoja ana Luku yake atalipa Sh. 3,000 sasa kwa nini huyu analipishwa Sh. 3,000 na mwingine Sh. 1,000 na ni vyumba saba vile vile.

"Kuna mtu ni mstaafu kama alivyosema mwenyekiti wa kamati kwa nini huyu anapewa adhabu hiyo, suala la msingi kuna watu wapo tayari kulipa hawajapewa umeme.

"Ninapendekeza serikali iongeze fedha kwenye Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ili kusudi wanaotaka umeme wapewe na muwekeze kwenye mfumo wa Luku ikiwezekana hili suala la kusanyaji mapato kwa mfumo huu tusubiri ili huu utaratibu usije ukashindwa kama ule wa TRA katika kukusanya mapato haya," alipendekeza.

Mbunge wa Kaliua, Aloyce Kwezi, aliiomba serikali izishauri kampuni za simu kama itawekezana angalau waachie Sh. 1,000 ziende kwenye TARURA kwa sababu barabara za vijijini ndiyo mishipa ya uchumi.

Mbunge wa Viti Maalum Neema Lugangila, alitaka pia itazamwe suala la tozo simu.

Awali, katika taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, iliyosomwa jana na Mwenyekiti wake, Sillo Baran, ikizungumzia kuhusu kodi hizo za majengo, ilisema ubunifu huo una lengo la kupanua wigo wa mapato ya serikali na kufanya ukusanyaji wa kodi kuwa rahisi.

"Uamuzi huu unaenda na Tamko la Serikali la awali la kurejesha ukusanyaji wa kodi hii kwa Serikali za Mitaa ambazo zina rasilimali watu katika ngazi zote za kukusanya kodi hii. Pamoja na ubunifu huu kuwa mzuri unakwenda kinyume na Sheria ya Kodi ya Majengo ambayo inaangalia majengo ambayo yako kwenye maeneo yanayotakiwa kulipa kodi hiyo," ilisema.

Taarifa hiyo ya kamati ilisema mapendekezo hayo yanachukulia nyumba zote zenye umeme hata zile ambazo ziko vijijini lakini hazipo kwenye maeneo ambayo kwa mujibu wa sheria hazina sifa ya kutozwa kodi.

Kamati hiyo ilisema mapendekezo hayo hayatoi msamaha kwa taasisi za umma na majengo mengine ya umma ambayo yanatumia umeme lakini kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Majengo yamesamehewa kodi hiyo.

"Kuweka kiwango mfano kwa nyumba zilizoko mjini na vijijini ni kuwaumiza wananchi ambao wanaishi vijijini. Kamati inaishauri serikali kwamba ubunifu huu uende sambamba na kufanya uthamini wa nyumba na kutumia Luku kama namba ya mlipa kodi na kila Luku itozwe kulingana na nyumba ambayo Luku hiyo ipo," alisema.



Rais Samia Suluhu Hassan akifungua koki ya bomba kuzindua mradi wa maji utakaohudumia mji wa Misungwi na maeneo ya pembezoni katika hafla iliyofanyika Misungwi mkoani Mwanza. **PICHA: IKULU**

# Kina maji chakwamisha Daraja la JPM

**Na Richard Makore,** MISUNGWI

KUONGEZEKA kwa kina cha maji katika Ziwa Victoria, jijini Mwanza kumechangia kazi ya ujenzi wa Daraja la JPM katika eneo la Kigongo- Busisi kuwa ngumu kutokana na wataalamu kulazimika kuongeza urefu wa mabomba na nguzo kwenda chini.

Akizungumza jana wakati wa ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan, kukagua daraja hilo jijini Mwanza, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Patrick Mfugale, alisema kuongezeka kina cha maji kumesababisha wataalamu kuanza kubadilisha mabomba na kuweka marefu kwenda chini tofauti na walivyokuwa wamepanga.

Alisema ujenzi wa daraja hilo lenye urefu wa kilomita 3.2 utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 714 na umefikia asilimia 27, huku kazi ikiwa ngumu kutokana na mabadiliko hayo.

Mfugale ambaye ni mhandisi kitaaluma, alisema ujenzi daraja la muda umekamilika na mkandarasi anafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha linakamilika ndani ya muda wa mkataba mwaka 2024, na kwamba litakuwa msaada kwa eneo la Kanda ya Ziwa na nchi jirani.

"Daraja hili linajengwa na mkandarasi kutoka nchini China na kazi hiyo inafanyika usiku na mchana," alisema.

Rais Samia alikagua daraja hilo kwa kupita kwa gari kuanzia upande wa Kigongo wilayani Misungwi hadi Busisi sehemu ya Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza.

Naye Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Leonard Chamurho, alisema baada ya daraja kukamilika magari yatakuwa yanatumia dakika nne kuvuka.

Akihutubia wananchi wa Misungwi baada ya kuzindua mradi wa maji wa zaidi ya Sh. bilioni 13, Rais Samia alionya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mkoani Mwanza (MWAUWASA), kuacha kuwabambikiza wananchi ankara za maji.

Alisema kuna tabia ya watumishi wa mamlaka za maji kutoa ankara za mwezi ambazo siyo sahihi. Aliongeza kuwa watumishi wa mamlaka za maji wakibambika ankara itachangia wateja wao kuanza kubuni njia za kukwepa kulipa.

Rais Samia aliwataka wananchi kulipa ankara za maji ili kuisaidia serikali kuendelea kutoa huduma kwa wananchi muda wote.

Kadhalika, alisema mradi huo utahudumia wananchi 64,208 na upatikanaji wa maji utakuwa umefikia asilimia 100, huku akiagiza kukamilika kwa miradi inayoendelea nchini.

Kwa upande wake, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema ili kuhakikisha miradi ya maji inatekelezwa wametimua wahandisi 118 na makandarasi 69 wababaishaji.

## Seth, Jamhuri wakubaliana

**Na Kulwa Mzee**

MKURUGENZI wa Kampuni ya Kufua Umeme (IPTL), Herbinder Seth na upande wa Jamhuri wamefikia makubaliano katika mazungumzo waliyokuwa wakifanya kwa ajili ya kumaliza kesi hiyo.

Akiiwakilisha Jamhuri, Wakili wa Serikali Mkuu, Martenus Marando, alidai hayo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jana wakati kesi hiyo ilipokuwa ikitajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

"Tumepitia kwa pamoja, tumefikia hatua ya kukubaliana kuhusu alicholalamikia au kuomba katika barua zake, sasa tunaendelea na shauri," alidai Wakili Marando.

Alidai upande wa utetezi kama hauna mtazamo mwingine anaomba shauri hilo lifike mahakamani kesho ili kuendelea na hatua zingine za usikilizwaji.Wakili wa Utetezi, Melchisedek Lutema, alidai huo ndio ukweli na ndio msimamo wa pande zote mbili.

Mahakama ilikubali maombi ya Jamhuri na kuahirisha kesi hiyo hadi kesho saa nne asubuhi kwa ajili ya kusikiliza kesi ama kumaliza kesi hiyo baada ya makubaliano.

Mazungumzo kati ya Seth na Serikali yalianza wiki iliyopita ambapo Wakili wa Serikali Mkuu, Marando alidai mshtakiwa aliandika barua mbalimbali kupitia mawakili wake kwa lengo la kufanya mazungumzo ya kumaliza shauri hilo.

HABARI KITAIFA

# Wenye namba za NIDA kupata Vitambulisho vya Taifa Agosti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi imesema ifikapo Agosti 2021, wananchi wote waliotambuliwa na kupewa namba za usajili watakuwa wametapatiwa vitambulisho vyao vya Taifa.

Pia katika kipindi cha miezi mitano (Januari 14- Mei 13, 2021), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imezalisha na kusambaza vitambulisho 7,148,971 katika wilaya 73 nchini.

Hadi kufikia mwezi Mei, 2021 Mamlaka imegawa Namba za Utambulisho (NIN) kwa wananchi 11,000,000 kutokana na mfumo wa NIDA kuunganishwa na mifumo mingine ya taasisi za serikali na binafsi.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Khamis Hamza Chilo, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Martha Mariki.

Mbunge huyo alitaka kujua ni lini serikali itakamilisha utoaji wa Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi kwa kuwa kumekuwa na tatizo la upatikanaji wake.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema kupitia mpango kazi wa kuzalisha vitambulisho inatarajiwa kuwa ifikapo Agosti, 2021 wananchi wote waliotambuliwa na kupewa namba za usajili watakuwa wamepatiwa vitambulisho vyao.

Alisema mpango huo unalenga kuzalisha vitambulisho kwa awamu kwa kila wilaya na kati ya vitambulisho vilivyotolewa katika wilaya 73, wilaya 63 ni Tanzania Bara, wilaya 10 ni kwa Zanzibar na kazi ya uzalishaji inaendelea.

Kadhalika wananchi wanaendelea kupata huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi kama za kifedha, kufungua biashara, kupata namba ya mlipa kodi (TIN), kupata hati ya kusafiria, umilikishaji ardhi na kusajili laini za simu kwa kutumia NIN wakati wakisubiri kupatiwa vitambulisho vyao vya Taifa.

Katika swali la nyongeza, Mbunge alisema miongoni mwa vigezo vinavyokwamisha kupata ajira ikiwamo mikoa inayopakana na nchi jirani kama Katavi na Kigoma ni ucheleweshaji na upatikanaji wa namba za NIDA.

"Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kutotumia kigezo hicho wakati vijana wanapoomba ajira ili wapate ajira? Kwanini mfumo usiunganishwe na wa RITA ili kuonesha ni raia wa kuzaliwa," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema serikali imeamua kuweka kigezo hicho ili kubaini wapi ni Watanzania na wasio na utanzania.

Alisema serikali imegundua kero hiyo itaendelea kutoa kipaumbele kwa vijana kupata vitambulisho kwa wakati.

Hata hivyo, alisema kuna vitambulisho vipo tayari kwenye baadhi ya maeneo, lakini wahusika hawajaenda kuchukua na kutoa wito kwa wananchi kufika kwenye ofisi hizo kuchukua vitambulisho vyao.

## Mufti ataka kasi kesi viongozi wa Uamsho

**Na Elizabeth Zaya**

MUFTI wa Tanzania, Shekhe Aboubakar Zuber, ameziomba mamlaka zinazohusika na kesi inayowakabili viongozi wa Uamsho iharakishwe kusikilizwa ili hatima yao ijulikane.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa mkutano wa viongozi wa dini waliokutana kwa ajili ya kujadili mambo mbalimbali yanayoendelea nchini.

Alisema ni miaka mingi sasa tangu kesi hiyo ianze kusikiliwa na kuomba wenye mamlaka ya kusimamia kesi kufanya haraka kusikiliza ili ifikie muafaka.

"Hatuwezi kuingilia mambo ya kisheria, lakini ninachoweza kuomba ni uharakishwaji wa kusikiliza kesi yao, kesi hii imekaa miaka mingi, suala hili niombe mamlaka husika ziharakishe kuisikiliza kwa sababu imekaa miaka mingi," alisema Mufti na kuongeza:

"Usikilizwaji wa kesi kwa haraka na hukumu ikatolewa itajulikana nani ana hatia gani na achukuliwe hatua gani na nani hana, kuliko kukaa ndani muda mrefu bila kufahamu hatma yao."

Miongoni mwa mambo mengine ambayo viongozi hao wa dini walizungumzia ni kuhusu vitendo vya ukatili vinavyoendelea kwa watoto na kuwataka wazazi kuwajibika katika malezi ya watoto wao.

"Hawa watoto ndiyo viongozi wa nchi tunaowategemea kesho, kwa hiyo tusipowajibika katika kuwatunza na kuwalinda tunakuwa tunaharibu taifa letu, ni vema kila mzazi, mlezi na jamii yote iwajibike katika kumlinda mtoto,"alisema Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT)Jimbo la Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa.

Alisema: "Asilimia kubwa ya watoto huharibika tabia kutokana na kukosa uangalizi wa wazazi ambao wanabanwa na shughuli za kila siku, hivyo wanapaswa watenge muda wa malezi. Tuombe kwamba kila unapobarikiwa kupata mtoto, uwajibike pia na katika kumlea na kumlinda."

Machi 28, mwaka huu Rais Samia Suluhu Hassan wakati akipokea taarifa ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ya mwaka 2019/2020, aliiagiza kuharakishwa kwa kesi, kuziondoa zisizo na msingi ili kuondokana na idadi kubwa ya kesi ambazo serikali imekuwa ikishindwa.




## Padri aipa moyo familia iliyopoteza watatu Dar

**Na Maulid Mmbaga**

FAMILIA iliyowapoteza watatu waliouawa na mfanyakazi wao mwishoni mwa wiki Masaki mkoani Dar es Salaam, imetakiwa kuendelea kufanya ibada na kuomba huruma ya Mungu juu ya waliowasababishia maumivu kwa kuwapoteza ndugu zao.

Mwili wa Emilly Mutaboyerwa na binti zake, Daniela (15) na Damita (13) ilifanyiwa ibada ya kuagwa katika Kanisa la Mtakatifu Martha Mikocheni.

Mama huyo na wanaye waliuawa Juni 9, mwaka huu, nyumbani kwao Masaki na anayedaiwa kufanya mauaji hayo ni Shadrack Kapanga (34), aliyekuwa mlinzi katika nyumba hiyo ambaye alikamatwa Juni 11, 2021 akiwa katika harakati za kutoroka.

Jana wakati wa ibada ya kuaga miili ya wanafamilia hao, Padri wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Martha Mikocheni jijini Dar es Salaam, Jorge Morales, aliwataka wanafamilia kumsifu na kumtumikia Mungu kwa moyo mkunjufu na waendelee kumuomba ili kupokea ibada za wapendwa wao waliopatwa na umauti, pia waendelee kuwaombea wale waliosababisha maumivu kwa ndugu zao.

"Mtukuzeni, msifuni, muabuduni Bwana na Mungu na mtumikieni kwa moyo ulio mkunjufu. Mji usipolindwa na Mungu walinzi wanakesha bure, tuombe huruma ya Mungu zaidi na mkono wake juu ya wale walio sababu ya maumivu yetu hasa yale maumivu yasiyo na faida," alisema.

Aliongeza kwa kuwataka wanafamilia kuomba huruma kwa wale ambao ni watesi wa maisha yao, lakini kwa namna ya pekee kwa wale wanafamilia ambao miili yao imejua maumivu hayo, na aliwasisitiza kuendelea kufanya ibada.

"Tunafarijiana sote, kwani tunaugua sote, kanisa linaugua, jamii inaugua, ndugu jamaa na marafiki wanaugua, majirani wanaugua hivyo tumuombe Mungu atusaidie kulipokea tukio hili kwa moyo mkunjufu," alisema.

## NIC yaidai serikali bil. 40/-

**Na Romana Mallya,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, imebaini Shirika la Bima la Taifa (NIC) linaidai serikali jumla ya Sh. bilioni 40.3, fedha ambazo ni kwa ajili ya kutoa bima kwa miradi mikubwa na ya kimkakati.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Sillo Baran, aliyasema hayo jana bungeni wakati akisoma taarifa ya kamati kuhusu hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2020, mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2021/22, tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2020/21 pamoja na mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka mpya wa fedha.

Alisema kamati imebaini kwamba pamoja na serikali kufanya uamuzi wa kulipa shirika hilo kazi hiyo lenyewe halina mtaji wa kutosha, hivyo kulazimika kuzitosa kwa njia ya mtawanyo.

Alisema kamati inaishauri serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina kuliongezea shirika hilo mtaji na kulipa madeni yote ambayo linaidai ili lijiimarishe na kufanya kazi kwa ufanisi.

# Serikali yasisitiza uvaaji barakoa kwenye mikusanyiko

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka wananchi kuchukua tahadhari ya maambukizi ya virusi vya corona kwa kuvaa barakoa kwenye mikusanyiko.

Dk. Gwajima alitoa tahadhari hiyo Juni 12, jijini Dar es Salaam kwenye uzinduzi wa mtambo wa kisasa wenye uwezo wa kufanya uchunguzi na matibabu ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Kwa dhamana niliyonayo naomba niwakumbushe kwamba katika mazingira kama hayo ambayo tunayokuwa tumesongamana kidogo ni vyema tukafanya matumizi ya hii kitu (barakoa), naomba niwakumbushe hilo na naamini mtatekeleza," alisema.

Akizungumza na waandishi wa habari, Dk. Gwajima alisema kamati iliyoundwa na Rais kushauri mwenendo wa masuala ya corona nchini ilisema nchi ipo salama na itaendelea kuwa salama.

"Ila tarehe 17 Mei, 2021, Brazil, India na nchi nyingine zilikuwa zinapigwa na wimbi la tatu, kwa hiyo ikasema kwamba hata sisi lazima tujitahadharishe na kujizatiti ili kuhakikisha haliingii kwetu hili wimbi la tatu, tusiliruhusu," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo kamati ilibainisha mikakati ya kukabiliana nalo.

"Sasa na mimi kwenye pitapita yangu leo nimeona, utasikia vyombo vya habari huko Uganda wanasema hali sio nzuri kwa takwimu zao, utasikia huko Congo hali sio nzuri na maeneo mengine kila siku yanaibuka, lakini Mungu kwetu anasaidia wataalamu wetu wa mipakani, viwanja vya ndege na wananchi wanaendelea kuchukua tahadhari," alisema.

Waziri Gwajima alisisitiza; "Tunapofika maeneo kama hapa tukakuta watu wamesongamana na Wizara ya Afya ilishasema hivi, pima mwenyewe kwenye msongamano au sio msongamano, sasa watu wanakaa kwenye msongamano bila barakoa, sijakwambia ukienda shambani kulima uvae barakoa."

"Sijakwambia ukae mahali penye mzunguko wa hewa wa kutosha uvae barakoa kwasababu tunasema huwezi kuvaa barakoa saa 24 kuna mazingira ukishafika kuna msongamano hewa haizunguki vizuri hapa lazima nivae barakoa tutembee nazo hata mimi natembea na yangu," alisisitiza.

Waziri Gwajima alisema hata Rais akienda eneo lenye msongamano huvaa barakoa yake.

"Tuvae barakoa misongamano inajulikana, tusiongezeane kazi, matamko tumeshayatoa na tunaendelea kutoa, kazi ya Wizara ya Afya ni kutoa elimu na wadau wake na kazi ya wananchi ni kupokea elimu na kutekeleza, kwa pamoja kama taifa tutaendelea kuwa salama kama tulivyodhibiti wimbi la kwanza na la pili, hata la tatu halitaingia," alisema.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, akionyesha jana kwa waandishi wa habari mali mbalimbali zilizokamatwa kwenye operesheni ya kupambana na uhalifu mkoani Iringa. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Rais Samia, vyama vya siasa wamlilia Prof. Baregu

**Na Salome Kitomari**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemwelezea mwanazuoni na aliyekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Profesa Mwesiga Baregu, kama msomi mzuri aliyesimamia alichokiamini. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffar Haniu, rais alitoa pole kwa familia na wengine walioguswa.

"Nitamkumbuka Prof. Baregu kama msomi mzuri aliyependa kusimamia kile alichokiamini na ambaye alilipenda taifa na kupenda siasa za kistaarabu," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Naye Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Itikadi na Uenezi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, katika taarifa yake alisema wamepokea kwa masikitiko na huzuni taarifa ya kifo cha mwanasiasa na msomi.

"Mwenyekiti wa CCM, Samia anatoa salamu za rambirambi kufuatia msiba wa mwanasiasa huyo aliyewahi kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, na kubainisha kuwa wakati wa uhai wake alifanya siasa safi akiongozwa na hekima, busara na fikra yakinifu za uzalendo na utaifa," alisema.

Katika taarifa yake hiyo, Mwenyekiti Samia alisema; "Profesa Baregu ni miongoni mwa wasomi na wanaharakati wa mwanzo walioamsha joto la kudai mfumo wa siasa za vyama vingi mwanzoni mwa miaka ya 1990, ni mwanasiasa aliyependa majadiliano na kufikia suluhu kwa njia ya kushauriana akitumia nguvu ya hoja, akiwa muumini mzuri wa demokrasia, siasa safi na misingi ya utawala bora."

Naye Katibu wa Habari, Uenezi na Mahusiano ya Umma, Salim Bimani, alisema alikuwa mwanazuoni mwenye msimamo usioyumba na mwanasiasa mwanataaluma mwenye kutumainiwa, aliyetoa mchango mkubwa katika harakati na mapambano ya ujenzi wa mabadiliko ya kisiasa na kikatiba.

"Alijitoa na kujitolea bila woga kuongoza mijadala yenye kushawishi na kutoa shinikizo la kutaka Tanzania irejeshe mfumo wa siasa za kiushindani katika miaka ya 1990, harakati zilizozaa matunda ya mfumo wa vyama vingi tulionao leo," alisema na kuongeza;

"Tutamkumbuka pia kwa umahiri wake wa ujenzi wa hoja alipokuwa miongoni mwa wajumbe kwenye Tume ya Mabadiliko ya Katiba. ACT-Wazalendo tunaamini kifo chake kimeacha pengo kubwa kutokana na umahiri na mchango mkubwa aliotoa."

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana, Juni 17 mwili utafanyiwa ibada nyumbani kwake Kunduchi, utasafirishwa Juni 18 na kuzikwa Jumamosi, kijijini kwake mkoani Kagera.

## HABARI KITAIFA



Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Najma Murtaza Giga, akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano mfupi uliofanyika katika ofisi za OSHA za Dar es Salaam wakati wa ziara ya kamati hiyo mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. **NA MPIGAPICHA WETU**

# CTI: Bajeti imezingatia mchango wa wadau

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda nchini (CTI), limeelezea kufurahishwa na bajeti ya serikali kwa kuchukua michango mingi waliyoitoa wakati wa maandalizi ya bajeti hiyo ikiwamo kufuta tozo mbalimbali.

Mwenyekiti wa Shirikisho hilo, Paul Makanza, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye ofisi za CTI kuhusu wenye viwanda walivyoipokea bajeti hiyo.

Alisema CTI inaamini kama bajeti hiyo itatekelezwa kama ipasavyo sekta ya viwanda itakua na kukuza pato la taifa na kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni huku akiahidi kuwa wenye viwanda watashirikiana vyema na serikali.

Alisema wakati wa mchakato wa kuandaa bajeti hiyo wenye viwanda walipeleka mapendekezo mengi na kwa kiwango kikubwa yamechukuliwa hali ambayo itavisaidia viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji na kuongeza ajira.

Alisema, hatua ya serikali kupunguza kodi kwenye mshahara kutoka asilimia tisa mpaka nane kutawasaidia wafanyakazi kuongeza kipato chao huku akisifu uamuzi wa serikali wa kupunguza gharama za matangazo ya baishara na mabango.

Alisema hatua ya kuondoa asilimia 15 ya sukari ya viwandani waliyokuwa wakitoa wazalishaji wa sukari kutawaondolea mzigo wenye viwanda hivyo kuongeza uzalishaji na kuwaondolewa usumbufu uliokuwapo.

Makanza alisifu hatua ya serikali kupunguza tozo ya OSHA kutoka Sh. 590,000 hadi 150,000, tozo ya Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira kutoka Sh. 1,000,000 hadi Sh. 100,000 ya kuteketeza dawa zilizopita muda wake kumewapunguzia mzigo mkubwa wazalishaji na wafanyabiashara.

Pia alisema iwapo bajeti hiyo itatekelezwa kama ilivyopangwa, itasaidia kwa kiwango kikubwa kujenga Tanzania ya viwanda huku akiahidi kuwa CTI itakuwa bega kwa bega na serikali kuhakikisha ndoto ya Tanzania ya viwanda inafikiwa.

# Polisi yanasa mfungwa aliyetoroka gerezani

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JESHI la Polisi Mkoa wa Iringa limewakamata watuhumiwa 23 wa makosa mbalimbali, akiwamo mfungwa aliyetoroka gerezani.



Pia limekamata mali mbalimbali zinazodhaniwa za wizi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Juma Bwire (pichani), alisema jana kuwa operesheni hiyo endelevu imefanyika katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Iringa.

Kamanda Bwire alimtaja mfungwa aliyekamatwa baada ya kutoroka Gereza la Isupilo kuwa ni namba 1979 /2019 Denis Ngumbi, ambaye alikuwa akitumikia kifungo cha miaka minne jela.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Jun 3, mwaka huu majira ya asubuhi katika Kijiji cha Igowole wilayani Mufindi.

Katika tukio lingine, alisema wamewakamata watuhumiwa Ernest Muhume (67) na Lucas Muhume (50), ambao walisalimisha bunduki tatu aina ya gobore.

Kadhalika, wamekamata mali mbalimbali ikiwamo TV, simu, laptop, spika, mizani, majiko ya gesi, vinywaji aina mbalimbali na mali nyingine nyingine.

Kamanda Bwire alisema Juni 11, mwaka huu katika eneo la Ngome Kihesa katika Manispaa ya Iringa, walimkamata Tyson Ngailo (28), fundi simu akiwa na laptop, tablet internet na vifaa vingine vinavyodhaniwa ni mali za wizi.

Kwa mujibu wa Bwire, Jeshi la Polisi limewakamata watuhumiwa kadhaa kwa makosa ya wizi, kupatikana na pombe aina ya gongo, matumizi ya bangi na kupatikana mali kwa njia za udanganyifu.


## UUZAJI WA MALI

**Mwaliko wa zabuni**

Benki ya Stanbic Tanzania inakukaribisha katika zabuni ya wazi.

- Zabuni zitafunguliwa tarehe 22 Juni 2021. Wazabuni au wawakilishi wanakaribishwa kuhudhuria tukio la ufunguzi litakalofanyika saa 9.00 mchana, katika ukumbi mkuu wa mkutano, makao makuu ya benki ya Stanbic, iliyopo katika makutano ya barabara ya Ali Hassan Mwinyi na Kinondoni.
- Zabuni zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji, Stanbic Bank (T) Ltd, S.L.P. 72647, Dar es Salaam. Zabuni zionyeshe wazi kuwa ni kwa ajili ya ununuzi wa lori, trela ,vifaa vya magari au mashine.
- Zabuni zote ziambatanishwe na ada ya malipo isiyorejeshwa ya shilingi 50,000/=; aidha kwa mfumo wa cheki au fedha iliyowekwa kwenye akaunti ya benki ya Stanbic na risiti iambatanishwe pamoja na nyaraka za zabuni. Jina la akaunti ni Sundry Deposit Suspense ACCOUNT NO. 121000TZS5108001.
- Zabuni ziwasilishwe kwenye sanduku la zabuni lililo kwenye eneo la mapokezi.
- Bidha zinaweza kukaguliwa katika maeneo yafwatayo: Magari yote yanapatikana Dar es Salaam, tafadhali piga 0746 969 693 kupata taarifa zaidi. Mashine inapatikana Songea CBD, tafadhali piga 0769 210 979 kupata taarifa zaidi.
- Mzabuni atapaswa kulipa asilimia 25 baada ya kutangazwa kukubalika kwa zabuni yake na salio linalobakia lilipwe ndani ya siku 7.
- Benki inaweza kukubali zabuni yoyote na haina wajibu wa kuelezea sababu zake.
- Bidhaa zitauzwa "kama zilivyo" baada ya mnunuaji kupitia na kuridhishwa na hali ya bidhaa kabla ya kununua.
- Ushindi wa zabuni hautajali ukubwa wake. Benki ndio yenye maamuzi ya mwisho.
- Zabuni ipo wazi kwa jamii yote. Mtu yeyote anaweza kuomba zabuni moja au zaidi.

**Magari:**

| AINA | MODELI | MWAKA WA USAJILI | USAJILI/NAMBA YA USAJILI | MAHALI ILIPO HIFADHIWA | GHARAMA TENGEFU |
|---|---|---|---|---|---|
| ZHONGTONG | LCK6120A | 2014 | T 169 DCA | BILO STAR MBEZI BEACH YARD | 19,000,000.00 |
| ZHONGTONG | LCK6120A | 2014 | T 161 DCC | BILO STAR MBEZI BEACH YARD | 25,000,000.00 |

**Mashine:**

| AINA | MODELI | MAELEZO | USAJILI/NAMBA YA USAJILI | GHARAMA TENGEFU |
|---|---|---|---|---|
| LIAO YUAN | QLB80 | MOBILE ALSPHALT BATCHING PLANT | 16020606 | USD 208,000 |

Stanbic Bank IT CAN BE™

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunatarajia makubwa mjadala bajeti 2021/22

**JANA** wabunge walianza mjadala wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2021/22, ambayo ndiyo wakati wa wawakilishi wa wananchi kwenye muhimili huo kutoa maoni na mapendekezo yao.

Kwa tafsiri halisi ni kuwa sasa wananchi wanashiriki kujadili bajeti hiyo kwa maana ya kwamba kama ni mbunge wa jimbo anawasemea waliomchagua na ambao hawakumchagua wakati wa uchaguzi mkuu mwaka 2020.

Pia wabunge wa makundi ya wafanyakazi, mashirika yasiyo ya kiserikali, wenye ulemavu wateule wa rais na viti maalum wote kwa ujumla wanawajibu wa kujadili kwa kutoa maoni na mapendekezo katika kilichopendekezwa na serikali.

Bajeti ilisomwa Ijumaa na wabunge walipewa siku tatu za kusoma na kuanza mjadala, ambao kabla umetanguliwa na taarifa ya kamati ya bajeti kutoa mapendekezo yake.

Matarajio ya wananchi ni mjadala mzito ambao utagusa maeneo yote ya msingi kwa jicho la pekee, kwamba mbunge atumie vyema dakika 10 atakazopewa kwa ajili ya kuchangia.

Kwa siku saba wabunge watakuwa na wajibu wa kujadili bajeti hiyo, maana yake ni kuwa kila jimbo litapata uwakilishi na Watanzania watakuwa wamesemewa kupitia wawakilishi hao.

Wananchi wanachotaka kusikia ni hoja zenye mashiko, kwa kuangalia vikwazo vilivyopo vinavyogusa moja kwa moja. Mathalani, kama kwenye masuala ya maji, miundombinu na huduma za afya hasa upatikanaji wa dawa na bima ya afya kwa wote.

Haitarajiwi mbunge atumie dakika zake kupongeza wapigakura, kusifia wenye mamlaka, kutaja familia yake badala yake atoe hoja zenye mashiko kwa umma kwa ujumla.

Haya yote yalishafanyika tangu bunge la Novemba na sasa ni mwendo wa kufanyakazi ambayo imeewafanya wawepo ndani ya muhimili huo muhimu wa kutunga sheria na kuishauri serikali.

Kwamba, bajeti inazungumzia kodi mpya ya laini za simu, miamala na kodi ya majengo kwa kutumia Luku za umeme.

Je, ni kwa namna gani itakwenda kutekelezwa, waishauri serikali vyema ili kuondoa au kumaliza malalamiko ambayo huenda yakajitokeza?

Kwa hoja zenye mashiko maana yake serikali italazimika kufafanua kwa kina ili wananchi waelewe utekelezaji.

Tunaamini wabunge walisoma na kuelewa ikiwamo kutafuta wataalamu mbalimbali wa kutafsiri au kufafanua kile kilichopo kwenye bajeti, ikiwamo kubeba maoni ya wananchi wa kawaida, wasomi na kada mbalimbali, ili kitakachozungumzwa isiwe ni fikra ya mbunge.

Tunatarajia siku saba zitakuwa ni za kushusha nondo za wananchi katika kuichambua bajeti, ili utekelezaji unapoanza uwe rahisi zaidi kuliko kuwa na mkwamo wa hapa na pale.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# 'Twisheni' inaanza kurejea kinyemela



Na Sabato Kasika

**BAADA** ya malalamiko kutoka kwa baadhi ya wazazi na walezi kuhusu utozwaji wa fedha kwa masomo ya muda wa ziada au 'twisheni', serikali ilipiga marufuku ufundishaji huo katika shule za msingi na sekondari.

Ilipiga marufuku masomo ya ziada shuleni kwa kuwa yanazorotesha elimu na pia ni njia ambazo baadhi ya walimu hujikusanyia mapato na si kukuza elimu.

Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam, Elizabeth Thomas, aliwahi kukaririwa na vyombo vya habari akielezea kingine zaidi ambacho wamekibaini.

Kwa mujibu wa maelezo yake, kilichogunduliwa ni kwamba, walimu walikuwa wakifanya uzembe kufundisha darasani ili wawashawishi wazazi na walezi wa wanafunzi kutenga muda wa masomo ya ziada.

Kutokana na mazingira hayo, serikali ikazuia masomo ya ziada katika shule za umma, badala yake walimu wafanye kazi yao inavyotakiwa ili kukuza taaluma kwa wanafunzi.

Si hapo tu, bali 'twisheni' inaweza kusababisha wanafunzi ambao wazazi na walezi hawana uwezo kifedha, kurudi nyuma kielimu, kwa kuwa wenzao wanapiga hatua kutokana na masomo ya ziada ambayo wao hawapati.

Pamoja na tuisheni kuzuiwa katika shule za umma, inaelezwa kuwa baadhi ya walimu wameanza kuirejesha kunyemela na kutoza wazazi na walezi fedha kana kwamba serikali imeruhusu utaratibu huo.

Baadhi ya wazazi na walezi wa jijini Dar es Salaam wameanza kupaza sauti wakilalamikia kuwapo kwa 'tuisheni' iliyozoiliwa katika shule za umma, kwa kuwa ni kama zinabagua wale ambao hawana uwezo wa kulipa.

Wanaoguswa wanadai kuwa watoto wao wasipokwenda shuleni na Shilingi 300 kila siku, huchapwa au kuzuiliwa kupata masomo ya muda wa ziada, hali ambayo kwa namna moja au nyingine inaweza kuwakwamisha kielimu.

Wanadai kuwa kutoa masomo katika muda wa ziada ni 'biashara', ambayo inaweza kusababisha baadhi ya wanafunzi kukwama, hivyo wanaomba serikali kutoa kauli ili kuondoa utata uliopo sasa.

Kama ndivyo ilivyo sasa, basi ingependeza kama walimu watatumia muda wa vipindi vya shule, kufundisha kadri ya uwezo na ujuzi wao masomo mbalimbali ili kuwasaidia kielimu badala ya kuegemea biashara. Masomo ya ziada yana umuhimu wake, mojawapo ikiwa ni kumsaidia mwanafunzi kukuza uelewa, ufahamu na kuongeza ufaulu, lakini tatizo ni kwamba yamegeuka kuwa biashara.

Kwa mazingira yalivyo sasa, wanafunzi ambao wazazi na walezi wao hawana uwezo wa kulipa shilingi 300 kila siku kwa ajili ya masomo hayo ya muda wa ziada wanawezaje kukuza uelewa, ufahamu na kuongeza ufaulu?

Baadhi ya wazazi walishawahi kulalamika kuwa masomo hayo ni mzigo kwao, kutokana na baadhi ya walimu kuacha kufundisha muda wa kawaida wa masomo na badala yake kuelekeza nguvu kwenye mfumo huo.

Walimu kuelekeza nguvu katika mafunzo ya ziada kunatajwa kuwa mzigo kwa wazazi, kwa kuwa wanalazimishwa kuchangia fedha, ili watoto wao wahudhurie twisheni kwa mwalimu yule yule anayewafundisha. Baadhi ya wadau wa elimu wamekuwa wakiweka wazi kuwa, shule ambazo zinafundisha masomo ya ziada, zinaweza kufafanya vizuri katika mitihani, ingawa tatizo ni hilo la kutenga wanafunzi wasio na fedha.

Ingekuwa vyema iwapo walimu wakaelekeza nguvu zao katika kufundisha darasani muda wa kawaida wa masomo, ili kusaidia wote badala ya mtindo wa kutoza fedha ambazo ni kama ubaguzi kwa kaya zisizo nacho. Ikumbukwe kuwa sera ya elimu bure imeongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa na wanaoendelea na masomo baada ya kusajiliwa kuanza masomo katika shule mbalimbali.

Wote hao wanahitaji kufundishwa kadri inavyowezekana ili waelewe, lakini unapokuja mtindo wa masomo ya ziada, ambao unagawa makundi mawili ya wenye nacho na wasio nacho, basi wapo wanafunzi wanaokwama kielimu.

Elimu bure pia imesaidia kuinua uchumi wa Watanzania wa kipato cha chini, kwa kuwa fedha zilizokuwa zikitumika kwa ajili ya ada, sasa zinaweke-zwa kwenye mambo mengine ya maendeleo.

## Wachumi waeleza siri ya kuupaisha uchumi

**Na Romana Mallya,** DODOMA

PROFESA mbobezi katika uchumi, Prof. Samuel Wangwe, amesema kama serikali haitawekeza katika uchumi jumuishi kwa kuinua shughuli za kilimo, uchumi utaonekana umekua wakati wananchi wake wakiendelea kuwa maskini.

Aliyasema hayo juzi jijini Dodoma wakati wa majadiliano ya wabunge kuhusu masuala ya uchumi yaliyowahusisha wataalamu mbalimbali katika eneo hilo.

Akizungumzia eneo la uchumi shirikishi katika mkutano huo, Prof. Wangwe alisema ni lazima serikali ijielekeze kuchochea uzalishaji kwa sababu haitawezekana kujenga uchumi wa viwanda kama sekta ya kilimo itabaki kuwa duni.

"Tuongeze thamani ya mazao ambayo ndiyo yatagusa viwanda. Uzoefu wa mwaka 1970 kitu kimojawapo kilichoangusha viwanda ni udhaifu wa kilimo na mkakati wa kilimo ulipoandika ulisema utafuata baadaye, lakini haukufuata kwa hiyo viwanda vikaenda chini, kilimo ni kiunganishi cha uchumi wa viwanda," alibainisha.

Prof. Wangwe alitaja eneo lingine ni kurasimisha uchumi usio rasmi ili kuongeza tija na kipato kwa sababu watakuwa walipa kodi wazuri.

Alitaja takwimu za ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zinaonyesha kati ya mwaka 2012 na mwaka 2019 umaskini umepungua kutoka asilimia 28. 2 kufikia asilimia 26.1. Alisema maana yake uchumi unatakiwa kukua na umaskini kupungua na sekta nyingine kama viwanda na huduma ziibuke na siyo kilimo peke yake.

# Kamati yashauri mitaala ya elimu kupitiwa upya

**Na Romana Mallya,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imesema licha ya ubora wa miundombinu na ongezeko la idadi ya wahitimu wa elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu, bado kuna tatizo la aina ya ubora wa elimu kutokana na kutotoa fursa ya kumjenga mwanafunzi kujiajiri.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Sillo Baran, aliyasema hayo jana bungeni wakati akisoma taarifa ya kamati kuhusu hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2020, mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2021/22, tathmini ya utekelekeza wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2020/21 pamoja na mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka mpya wa fedha.

Alisema kamati hiyo inaishauri serikali kupitia upya mitaala yote na kuiboresha ili kuwawezesha wanafunzi kuanzia ngazi ya elimu ya msingi na sekondari kupata mafunzo ya stadi za kazi katika taaluma mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri wenyewe na kuajiriwa katika viwanda kwa kada ambazo zinahitaji watumishi wengi.

**BANDARI**

Baran alisema serikali ilieleza kamati kuwa Mamlaka ya Bandari ya Dar es Salaam (TPA), imeanza kuhudumia baadhi ya bandari bubu 693 kwa kuweka miundombinu muhimu za shughuli za kijamii na kibiashara kwa kuwa zilikuwa zinapitisha shehena kubwa bila kutambuliwa na baadhi kukosesha mapato na kuhatarisha usalama mipakani.

Alisema ni vyema serikali ikatafuta suluhisho la kudumu ili kutatua matatizo ya upotevu wa mafuta bandarini na kwenye bomba linalosafirisha mafuta kutoka bandari kwa kukamilisha haraka matengenezo ya Flow Meter bandarini na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa bomba linalosafirisha mafuta ili kubaini endapo kuna hujuma zozote.

**KILIMO**

Kamati hiyo imetoa mapendekezo 11 ikiwamo upatikanaji wa pembejeo, zana za kilimo na mbegu bora kwa wakati na kwa gharama nafuu, kudhibiti ubora wa pembejeo za kilimo na kuimarisha masoko ya mazao.


Pia kamati imependekeza kuweka mazingira wezeshi katika uwekezaji kwenye mnyororo wa thamani, kuhamasisha kilimo cha mkataba na kilimo kitalu na kuboresha upatikanaji na mifumo endelevu ya masoko ya mazao ya kilimo kwa kuboresha miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo.

Kadhalika, imependekeza kuboresha mifumo ya upatikanaji wa taarifa za masoko ya mazao na kuongeza mauzo ya mazao na bidhaa za kilimo ndani na nje ya nchi, upatikanaji wa mitaji, kuboresha miundombinu na teknolojia.

Pia kuimarisha taasisi za utafiti wa kilimo, vyuo vya mafunzo ya kilimo, ufundi stadi, udhibiti wa ubora wa pembejeo na zana za kilimo, kujengwa maabara za kutoa ithibati ya mazao ya kilimo.

**UVUVI**

Kamati imetoa mapendekezo sita ambayo ni kuweka vivutio maalumu kwa wawekezaji wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, mazingira bora ya kuhamasisha wananchi kufuga samaki na kuhakikisha vifaranga vya samaki, chakula cha samaki na vifaa vya uvuvi vinapatikana kwa bei nafuu.



BYRNECUT OFFSHORE TANZANIA LIMITED
(Incorporated in United Republic of Tanzania)
Registration No. 105147

CERTIFIED EXTRACT OF THE SPECIAL RESOLUTIONS PASSED AT THE EXTRAORDINARY GENERAL MEETING OF THE MEMBERS OF THE COMPANY ON 20TH DAY OF APRIL 2021

**WHEREAS** the Directors of the Company have presented Certificate of solvency and proposed cancelation of shares and reduction of the share capital of the company, the following **special resolutions** were passed at the duly constituted Extraordinary General Meeting (EGM) of the Company held on 20th day of April 2021:

**RESOLVED THAT** 395,097,407 Shares of TZS 20 each held by Byrnecut Offshore PTY Ltd be cancelled from the shares of the Company.

**RESOLVED FURTHER THAT** upon the cancellation of 395,097,407 shares of the company, the share capital of the company be accordingly reduced by TZS 7,901,948,140 which equivalent to 395,097,407 Shares of TZS 20 each to reflect the cancellation of shares therein and that the remaining shares of the company shall be reconstituted and shall form the full shares of the company.

**RESOLVED FURTHER THAT** the changes be filed with the relevant Authorities in compliance with the law.

CERTIFIED TRUE EXTRACT

Chairman:
Name: GREGORYJACKSON

Secretary:
Name: IBRAHIM MAGA

BYRNECUT OFFSHORE TANZANIA LIMITED 105147




# Hukumu ya Mdude Juni 28

**Na Grace Mwakalinga,**

MBEYA

MATUMAINI ya wanachama na wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ya kupata hukumu ya mwanachama mwenzao, Mdude Nyagali, yamefifia baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya kuahirisha mpaka Juni 28, mwaka huu.

Jana wafuasi wa chama hicho wakiongozwa na viongozi wao, walifurika nje na ndani ya viunga vya mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya kufuatilia hukumu ya kesi hiyo ya kusafirisha dawa za kulevya inayomkabili Mdude.

Wanachama hao ambao baadhi walikuwa wamevalia sare za chama hicho walikuwa na matumaini ya wanachama mwenzao kusomewa hukumu, lakini matumaini hayo yaliyeyuka ghafla baada ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Zawadi Laizer kuahirisha.

Kabla ya hukumu hiyo kuahirishwa, wanachama hao walikuwa na nyuso zilizojaa matumaini, wakipiga stori na kucheka, lakini baada ya hakimu kuahirisha walitoka mahakamani hapo wakiwa na sura zenye huzuni huku baadhi wakinung'unika.

Hakimu Mfawidhi wa mahakama hiyo, Laizer alitumia dakika zisizozidi tano kutoa maelezo ya kuahirisha hukumu ya kesi hiyo na kutoa sababu zikiwamo ambazo ziko nje ya uwezo wake.

"Hukumu ya kesi hii sitaweza kuisoma kwa leo kwa sababu bado sijakamilisha kuiandika, lakini pia zipo sababu zingine ambazo ziko nje ya uwezo wangu, kwa hiyo naiahirisha kesi hii mpaka baada ya wiki mbili ambayo itakuwa Juni 28, mwaka huu," alisema Laizer.

Baada ya maelezo hayo ya hakimu, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe ambaye pia alihudhuria mahakamani hapo alifanya kazi ya ziada kuwapa matumaini wanachama hao akiwataka wawe na imani kuwa haki itatendeka dhidi ya mwenzao hata kama itachelewa.

Aliwaomba wanachama kuendelea na moyo wa upendo kujitokeza kwa wingi kusikiliza kesi ya mwenzao na kuwasisitiza kuwa Juni 28, wajitokeze tena kwa wingi mahakamani hapo.

Akitoa ufafanuzi wa kesi hiyo, wakili wa upande wa utetezi, Faraji Mangula, alisema uamuzi wa mahakama wameupokea kutokana na sababu zilizotolewa kwamba hukumu bado haijawa tayari.

Alisema upande wa utetezi hauna pingamizi lolote na uamuzi huo na kwamba majukumu yao walishayamaliza kilichobaki ni kusikiliza hukumu ambayo inatolewa na mahakama huku akiomba tarehe iliyopangwa hukumu itolewe bila kuwapo kwa sababu yoyote.

Mdude amekaa mahabusi tangu Mei 2020 hadi sasa akituhumiwa na kesi ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin gramu 23.4.




Ofisa Uhamiaji Mfawidhi wa Kituo cha Namanga, Mrakibu wa Uhamiaji, Prolimina Tairo, akitoa maelezo kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, juu ya sehemu ya kupimia afya kwa wageni wanaoingia na kutoka nchini wakati wa ziara ya kuimarisha doria na misako ili kudhibiti wimbi la wahamiaji haramu wanaoingia na kukamatwa nchini. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

## Bil. 8/- za TADB zapiga jeki alizeti

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) imeshatoa mikopo inayofikia shilingi bilioni 8.2 kuinua zao la alizeti katika mkoa wa Singida sambamba na kuleta mageuzi makubwa katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi nchini.

Akizungumza na waandishi baada ya mkutano wa wadau wa zao la alizeti, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema benki yake imejipanga kuhakikisha zao la alizeti linatoa mchango stahiki ikiwamo uzalishaji wa mafuta kula kwa wingi.

"Kama benki tumejipanga kuhakikisha zao la alizeti linatoa mchango mkubwa, hivyo tumeshatoa cha shilingi bilioni 2.2 kufanikisha ununuzi wa zao hilo hapa Singida," alisema Justine.

Akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya benki na juhudi zinazofanywa na benki hiyo mkoani hapa kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Justine alisema benki hiyo imejipanga kuwa wakulima wa zao la alizeti wananufaika na zao hilo ikiwamo kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima na kuinua pato la taifa.

"Kwa kushirikiana na benki washirika tunaahidi kuwezesha ununuzi wa zao hili ili wakulima waweze kunufaika na viwanda viweze kuzalisha mafuta kwa wingi hapa nchini," alisema Justine.

"Kumekuwa na changamoto ya ucheleweshaji wa kurejesha mikopo kwenye vyama vya ushirika (AMCOS), kwa mfano Manyara kuna Amcos za mahindi zaidi ya kumi ambazo tunazidai takribani shilingi milioni 500 huku bado wakisuasua kuzilipa," alisema.

# Hospitali Wilaya Kibaha yaanza kutoa huduma

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Jenifa Omolo, amewataka wananchi kufika katika Hospitali ya Wilaya ya Kibaha kupata matibabu badala ya kwenda katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi.

Omolo alisema kuwa hopitali hiyo ina waganga mabingwa wa kila aina pamoja na vifaa vya kisasa, huduma za dawa na waache kwenda kwenye vituo vyenye mrundikano wa wagonjwa kama kituo cha afya mkoani.

Alisema mwitikio bado ni mdogo wa wagonjwa kufika kutibiwa katika hospitali ya wilaya ya Lulanzi na kwamba jambo la kushangaza ni wagonjwa wengi kujazana kwenye Hospitali ya Tumbi na kituo cha afya cha mkoani.

Akizungumzia suala la usafi wa mazingira ambao umefanyika juzi kwenye hospitali hiyo, alisema watumishi wengi wamehudhuria na kufanya usafi ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya utumishi wa umma na watakuwa wakifanya usafi kila Ijumaa ikiwa ni sehemu ya kuhudumia jamii.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji Kibaha, Tulitweni Mwinuka, alisema kuwa moja ya madhumuni ya kufanya usafi ni kuijulisha jamii kuwa hospitali hiyo ni kwa ajili ya wananchi wa halmashauri na kabla hawajaenda Hospitali ya Tumbi ni vyema wakaanzia hapo kwakuwa huduma zote zinapatikana.

Mwinuka alisema kuwa baadhi ya huduma zinazotolewa ni pamoja na mionzi na kansa ya kizazi na wanafanya jitihada kuitangaza sehemu mbalimbali ili wananchi waweze kwenda kupata matibabu kwa kuwa huduma zinazotolewa ni bora kutokana na kuwa na wataalamu na vifaa vya kisasa.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Lulanzi, Silvanus Ndunguru, alisema wagonjwa wanaofika hapo ni kati ya 30 hadi 40 kwa siku.

Alisema wataalamu, dawa, vifaa tiba na chanjo ya kichaa cha mbwa zipo na huduma hiyo ilikuwa inapatikana jijini Dar es Salaam na vifaa tiba ni vya kutosha tatizo ni wateja.

Ndunguru alisema hospitali hiyo ilianza kazi baada ya mlipuko wa ugonjwa corona, mwaka jana na hapo ilikuwa kama kambi na baadaye ikaanza kutoa huduma za kawaida kama hospitali ya wilaya.

HABARI KITAIFA

## Chanzo ajira kwa watoto chaanikwa

**Beatrice Moses**

MIGOGORO kwenye ndoa na umaskini ni miongoni mwa mambo yanayotajwa kuwa chanzo cha watoto kuingia kwenye majukumu ya kutafuta kipato (ajira utotoni), hivyo kusababisha baadhi yao kushindwa kuendelea na masomo.

Meya wa Manispaa ya Ubungo, Jaffari Nyaigesha, aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya kutokomeza ajira kwa watoto yaliyoandaliwa na mtandao wa kudhibiti ajira kwa watoto.

Nyaigesha alisema migogoro hiyo inasababishwa na mambo kadhaa ikiwamo kukosekana kwa uvumilivu miongoni mwa wanandoa pamoja na kusahau au kutozingatia utekelezaji wa majukumu yanayomhusu kila mmoja.

Alisema kuwa serikali nayo imekuwa ikifanya juhudi katika kuwahudumia watu maskini kupitia mradi maalum wa TASAF, hivyo vyema kuendeleaza juhudi za kuwakomboa watoto, pia wazazi wapate muda mzuri wa kutafakari, kabla ya kuachana, ni vyema wawe wana tafakari hatima ya watoto.

Mratibu wa mtandao huo, Scholastica Pembe, alisema serikali pamoja na juhudi adha inazofanya inapaswa iangalie bajeti inawekwa kwa kiwango gani kwa ajili ya watoto na zinaingizwa namna gani katika utekelezaji.

## Salma Kikwete ataka mfuko wa korosho

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI imeshauriwa kurejesha mfuko wa kuendeleza zao la korosho kuwawezesha wakulima kuondokana na ucheleweshaji upatikanaji wa pembejeo mapema.

Imeelezwa pia kwamba kuwapo kwa mfuko kutawawezesha wakulima kupulizia mikorosho yao kwa wakati.

Ushauri huo ulitolewa na Mbunge wa Mchinga mkoani Lindi, Salma Kikwete, wakati wa kikao cha wadau wa korosho.

Akiwasilisha ombi la wakulima kutoka mikoa inayolima zao hilo, mbunge huyo alisema kurejeshwa kwa mfuko huo kutachangia wakulima kupata dawa kwa wakati.

Salma alisema korosho ni miongoni mwa mazao muhimu katika ustawi wa Taifa, kwani huchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa.

Aidha, aliwataka wakulima wa korosho na ufuta wasidanganywe juu ya kuondoa utaratibu wa kuuza mazao hayo kupitia stakabadhi ghalani kwani ndio mkombozi na faida kwa upande wao.

"Ninachowaomba ndugu zangu wakulima, wasije watu wakawadanganya eti mjiondoe kwenye mfumo huu, kwani una faida kwenu," alisema Salma.

# Maofisa ugani kuwa na mashamba darasa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kuhakikisha maofisa ugani wote wanakuwa na mashamba darasa kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wakulima katika maeneo yao. "Maofisa ugani lazima wawe na mashamba kwa ajili ya kufundishia wakulima na anayeshindwa kuonyesha shamba huyo hafai kuwa ofisa ugani."

Ametoa agizo hilo Jumapili wakati akizungumza na wadau wa zao la alizeti mkoani Singida.

Waziri Mkuu alisema wananchi waliacha kulima kwa sababu elimu ilikuwa haiwafikii, hivyo aliwaagiza wakuu wa wilaya katika maeneo yote yanayolima alizeti wasimamie uundwaji wa vikundi vya wakulima wa zao hilo.

"Vikundi ndio njia rahisi ya kuwafikia wakulima iwe kwa kuwapa elimu au mikopo," alisema na kuendelea:

"Hakikisheni mnakuwa na kanzi data za wakulima katika maeneo yenu. Kanzi data hiyo itawawezesha kujua idadi ya wakulima, ukubwa wa mashamba yao pamoja na mahitaji yao. Pia jengeni utaratibu wa kuwatembelea wakulima ili kujua changamoto zinazowakabili na kushirikiana nao katika kuzitafutia ufumbuzi."

Naye Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema wizara imejipanga katika kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 344 za sasa hadi kufikia wastani wa tani 2,000 hadi 2,500 kwa mwaka, hivyo ndani ya miaka mitatu ijayo nchi itakuwa imejitosheleza kwa mahitaji ya mbegu bora za alizeti.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, aliiomba serikali kuunda bodi itakayosimamia mazao ya mafuta ili kuboresha usimamizi wa mazao hayo.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Elibariki Masuke (kulia), na Mkuu wa Masoko na Mawasiliano, Neemarose Singo (kushoto), kutoka Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) wakipeperusha bendera kuashiria kuzindua huduma ya mwanzo wa kampeni ya Twende Sawa na NBC inayolenga kuwafikia wafanyabiashara wanaochipukia nchi nzima na kuwasogezea akaunti ya Kua Nasi mahusussi kwa wajasiriamali isiyo na gharama za uendeshaji pamoja na kuwapa elimu ya biashara wakiwa kwenye biashara zao. PICHA: JUMANNE JUMA

# Wabunge wafunguka utendaji wa OSHA

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amesema serikali imekuwa ikitegemea ushauri wa kamati za bunge kutekeleza mipango yake ipasavyo.

"Sisi kama serikali tunaweza tukawa tunajifungia ndani na kutengeneza mipango mbalimbali ya maendeleo, lakini ili mipango hiyo iweze kutekelezeka na kuwa na tija kwa wananchi tunategemea sana ushauri kutoka kwa wabunge hususan Kamati ya Katiba na Sheria, ambao ndio wawakilishi wa wananchi," alisema Mhagama mwishoni mwa wiki na wajumbe wa kamati hiyo wamefanya ziara katika ofisi za Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA).

Kamati ilijionea jinsi taasisi hiyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu inavyosimamia uzingatiaji wa viwango vya usalama na afya katika maeneo ya kazi.

Ziara hiyo imetokana na taarifa ya utekelezaji majukumu ya OSHA kwa mwaka 2020/2021 iliyowasilishwa kwenye kamati hiyo Machi mwaka huu ambapo iliridhishwa na utendaji, hivyo kuagiza kuandaliwa kwa ziara kwa ajili ya kuona uhalisia wa masuala ambayo wamekuwa wakiwasilishiwa kupitia taarifa mbalimbali.

Akizungumza baada ya kutembelea ofisi za OSHA, kiwanda cha Sigara (TCC) na kiwanda cha Gypsum cha Knauf (Knauf Gypsum Tanzania Limited) kilichopo Mkuranga mkoani Pwani, Kaimu Mwenyekiti Kamati hiyo, Najma Murtaza Giga, alisema wameridhishwa na kazi kubwa inayofanywa na OSHA katika kutoa miongozo ya kulinda nguvu kazi katika maeneo ya kazi.

"Suala tulilolifuatilia la usalama na afya mahali pa kazi kwa kweli hapa tumeona linazingatiwa ipasavyo, jambo ambalo linapelekea kampuni hii kufanya vizuri katika uzalishaji," alisema Giga.

Naye Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema kupitia ziara hiyo wajumbe wa kamati wamepata fursa ya kujionea hali halisi ya usalama na afya katika maeneo ya kazi nchini.

# TIC yatoa hati 499 kwa wawekezaji wa kigeni

BUNGE limeelezwa kuwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimetoa hati 401 kwa wawekezaji wa kigeni kuanzia mwaka 1999 hadi Mei mwaka huu.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), William Ole Nasha, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mafinga Mjini (CCM), Cosato Chumi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji mpaka sasa ni wawekezaji wangapi wamemilikishwa ardhi na kupata hati kupitia Kituo cha TIC. Akijibu, Ole Nasha alisema wawekezaji wa kigeni wanamiliki ardhi kwa ajili ya uwekezaji kupitia TIC kwa utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi namba nne ya mwaka 1999.

"Kifungu cha 20 cha Sheria hiyo kinaelekeza kwamba, Kamishna wa Ardhi atatoa hati ya umiliki wa ardhi kwa jina la TIC kwa ajili ya uwekezaji endapo uwekezaji huo unafanywa na mwekezaji wa kigeni," alisema.

Aidha, alisema kwa kutumia hati hiyo, TIC hutoa Hati ya Umiliki isiyo Asili kwa mwekezaji wa kigeni aliyewasilisha maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Alisema baada ya mwekezaji kupewa Hati ya Umiliki Isiyo Asili na TIC, hati hiyo inasajiliwa na Msajili wa Hati ambaye anatoa hati ya umiliki wa ardhi hiyo kwa jina la mwekezaji wa kigeni kulingana na masharti ya uwekezaji husika kama yalivyoainishwa kwenye mkataba wake na TIC.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema katika taarifa za Benki ya Dunia imetaja moja ya kero zinazowakabili wawekezaji ni upatikanaji wa hati kwa wakati, na utaratibu uliopo wa kamati ya kugawa ardhi inakaa mara nne tu kwa mwaka na kuhoji serikali kama ipo tayari kurahisisha kamati hiyo ikae hata kila mwezi. Akijibu, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Mkazi, William Lukuvi, alisema kwa sasa kamati ya kugawa ardhi kwa wawekezaji imeelekezwa kukutana kila mwezi badala ya miezi minne ili kurahisisha uwekezaji nchini.

"Ni kweli kwamba kanuni zilikuwa zinataka kamati hii ikutane mara nne kwa mwaka na ndivyo walikuwa wanafanya, lakini kutokana na ripoti ya benki na malalamiko ya wawekezaji na umuhimu wa kuharakisha uwekezaji nimelekeza sasa kamati hii ikutane kila mwezi badala ya miezi minne," alisema.

Alisema wakati huu wa serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, kamati imeanza kukutana mara moja kwa mwezi na katika kipindi cha Mei, kamati imekutana kila wiki jambo ambalo limesaidia maombi 173 kati ya 174 wawekezaji kupewa vibali na hati za uwekezaji.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akimsikiliza Mbunge wa kuteuliwa, Bashiru Ally, walipokuwa Bungeni jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Mabilioni yatengwa ujenzi barabara Mnivata-Masasi

SERIKALI imetenga Sh. bilioni tatu katika mwaka wa fedha 2021/22, kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya barabara ya Mnivata-Newala-Masasi yenye urefu wa kilomita 160.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini ujenzi wa barabara kutoka Mnivata hadi Masasi kupitia Newala kwa kiwango cha lami utaanza hasa kutokana na umuhimu katika kusafirishwa zao la korosho.

Akijibu, Naibu Waziri Kasekenya alisema barabara ya Mnivata-Newala-Masasi yenye urefu wa kilometa 160 ni sehemu ya barabara ya Mtwara- Nanyamba-Tandahimba-Newala-Masasi yenye urefu wa kilometa 210.

"Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mtwara-Nanyamba-Tandahimba-Newala-Masasi yenye urefu wa kilometa 210 umekamilika, ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo awamu ya kwanza ya sehemu ya Mtwara hadi Mnivata yenye urefu wa kilometa 50 imekamilika," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali kupitia kwa Wakala wa Barabara (TANROAD) inaendelea kuifanyika matengenezo mbalimbali barabara hiyo ili kuhakikisha kuwa inapitika majira yote ya mwaka.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 Sh. bilioni 1.017 zimetengwa kwa ajili hiyo.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema barabara hiyo ni muhimu kwa ajili ya usafirishaji zao la korosho na bajeti ya mwaka jana na mwaka huu na kuhoji lini serikali itatangaza zabuni ili apatikane mkandarasi atakayejenga barabara hiyo ya kilometa 210.

"Je, lini serikali pia itakamilisha kwa asilimia 100 kwa kipande kile cha kilometa 50 kilichojengwa?" Alihoji.

Akijibu, Kasekenya alisema baada ya kuanza kutumika kwa bajeti iliyopitishwa na bunge, zabuni ya kumpata mkandarasi itatangazwa ili ujenzi wa kipande hicho uanze.

## Uhaba watumishi kikwazo sekta afya

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta ya afya, ambapo hadi mwezi Mei mwaka huu watumishi waliokuwapo ni asilimia 41 ya mahitaji halisi.

Hata hivyo, serikali imetoa kibali kwa halmashauri nchini kuajiri watumishi wa afya kwa kutumia mapato ya ndani.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais hiyo, Dk. Festo Dugange, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Zodo.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali wa kukabiliana na tatizo la upungufu wa watumishi katika sekta ya afya ambayo kwa sasa ina upungufu wa watumishi 16,000.

Akijibu swali hilo, Dk.Dugange alikiri kuwa sekta ya afya nchini ina upungufu wa watumishi ambapo hadi mwezi Mei 2021 watumishi waliokuwapo ni asilimia 41 ya mahitaji halisi.

"Upungufu huu unatokana na sababu mbalimbali ikiwamo kustaafu kazi, kufariki na kuongezeka kwa idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini kutokana na utekelezaji wa programu ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya," alisema.

Aidha, alisema kuanzia mwaka 2017 hadi 2020 serikali kwa kushirikiana na wadau imeajiri watumishi 12,868 wa sekta ya afya ambao wamepangwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, alisema serikali inakamilisha taratibu za ajira 2,726 za watumishi wa kada mbalimbali za afya zilizotangazwa Mei 2021.

"Watumishi hao watapangwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vyenye uhitaji mkubwa, ili kukabiliana na changamoto hii, mpango wa serikali ni kuendelea kuajiri watumishi wa kada za afya kwa awamu," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge Zodo alitaka kujua mkakati wa serikali wa kuhakikisha kasi ya ujenzi wa vituo unaendana na kuajiri.

Dk. Dugange alisema serikali kutokana na kuthamani na kujali afya za wananchi imeendelea kujenga, kukarabati na kutanua vituo vya kutolea huduma za afya kwa lengo la kusogeza huduma bora za afya kwa wananchi.

"Serikali imeweka mkakati wa kuhakikisha kasi ya ujenzi wa vituo vya afya kote nchini inaendana na kasi ya kuajiri watumishi ili kuviwezesha vituo hivyo kutoa huduma katika vituo vyote vinavyojengwa na kukamilika," alisema.



Nipashe
# TESA
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Jumanne Juni 15, 2021


Ukurasa 12

## Wilaya inavyopigana kumaliza kero sugu ya madarasa mwakani


Ukurasa 14

## Bajeti hii ‘ilivyopitiwa’ na masuala haya muhimu

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

# Corona ilivyokatili watoto maelfu

## ■ Mwaka umeisha ukimya ukitawala

WAKATI dunia ikishuhudia athari za COVID-19, watoto wa Zanzibar kama ilivyotokea kwa mataifa mengine wameathirika na corona iliyosababisha kuyumba kielimu.

Katika kipindi cha kuanzia Machi 17 hadi Julai, 2020 shule zote zilifungwa kwa muda wa miezi mitatu lakini baada ya kufunguliwa baadhi ya wanafunzi wakikatisha masomo.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na wadau, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwahudumia Watoto (UNICEF), wamefanya utafiti kuangalia hali ya utoro Unguja na Pemba baada ya likizo ya corona.

**USHUHUDA WA MUZNE**

Maelfu ya wanafunzi wameacha shule utafiti huo umegundua kuwa takribani watoto 10,342 walikuwa hawajarejea shuleni na kwamba walitoka shule za maandalizi na msingi za Unguja na Pemba.

Kati ya hao wanaume walikuwa 5,570 na wanawake 4,772 ambayo ni hasara kwa taifa kwa vile serikali inagharamia elimu.

Muzne Kassim Hassan, ni miongoni mwa wanafunzi walioathirika, ambaye anaiambia Nipashe kuwa baada ya shule kufunguliwa Julai mwaka jana hakurejea shule na kukosa masomo kwa miezi tisa.

Kwa mwaka huu, Muzne angekuwa darasa la sita lakini alilazimika kurejea darasa la tano baada ya kukosa masomo muda mrefu, kutokana na kugeuzwa kuwa mlezi wa watoto wa jamaa zake.

Binti huyo awali aliishi na shangazi yake katika Kijiji cha Kitope Mkoa wa Kaskazini Unguja na baada ya shule kufungwa kujikinga na corona, mama yake mzazi alimrudisha nyumbani kwake Muungano mjini Unguja ili aishi na familia yao.



Wanafunzi wa Shule za Wilaya ya Mjini wakitumbuiza kwenye moja ya shughuli za kielimu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

“Baada ya shule kufunguliwa sikurejeshwa kwa shangazi alipokuwa naishi na kusoma tangu mwanzo ili niendelee na masomo, badala yake wakati wanafunzi wanarudi kuendelea na masomo nilibebeshwa mzigo wa kuwa mlezi wa ndugu zangu,” anasema.

“Nilikuwa namwambia mama shule zimefunguliwa anirejeshe kwa shangazi lakini hakutaka, nikaendelea kubakia nyumbani nikilea wadogo zangu,” anaongeza Muzne mwenye miaka 14.

Anasema sasa amefarijika kurudi shule na ameahidi kusoma kwa bidii ili kufaulu mitihani yake na kutimiza malengo yake ya kutaka kuwa rubani wa ndege za kitaifa na kimataifa.

**NGUVU IMEMRUDISHA**

Licha ya kurejea shuleni anasema: “Nahitaji kuungwa mkono kwa kusaidiwa vifaa vya shule kwa sababu familia yangu ni maskini.”

Muzne anasoma katika Shule ya Msingi Kitope baada ya jitihada za baba yake, walimu, uongozi wa wilaya ya kaskazini ‘B’ Unguja na maofisa wa ustawi wa jamii kuingilia.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kitope, Juma Abedi Muhammed, anasema mwanafunzi huyo ni miongoni mwa wengine 14, ambao hawakurudi shuleni baada ya kupungua kasi ya corona.

“Mwezi Julai shule zilipofunguliwa tena baada ya mapumziko marefu ya miezi mitatu wanafunzi 14 hawakurudi shule akiwamo Muzne. Wenzake walirejea baadaye baada ya kupata taarifa zao na kuwafuatilia,” anasema.

“Tulishindwa kupata taarifa za Muzne kwa sababu baba na mama yake wametengana, lakini baada ya kuarifiwa kuwa ametoroshwa shule na mama yake, tulishirikiana na serikali ikiwamo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini ‘B’ na kufanikiwa kumrejesha mwanzoni mwa mwezi wa Machi mwaka huu,” anasema.

**CORONA NA HOFU**

Muhhamed anasema corona iliposhika kasi wanafunzi wengi walipata mafua na homa kali na hilo liliongeza hofu hata baada ya shule kufunguliwa watoto wengi walihofia afya zao.

Anasema athari nyingine iliyojitokeza baada ya shule kufunguliwa ni ufundishaji ulikuwa mgumu kwa vile walikuwa nyuma sana kwenda sambamba na mpangilio wa kufundisha.

“Corona imeathiri sekta ya elimu kutokana na utoro wa wanafunzi na wengine hadi leo hawajarejea tena shuleni.” Anasema Mwalimu Mohammed.

**MSAKO WA SERIKALI**

Zuwena Hamad Omar, Ofisa wa Wanawake na Watoto Wilaya ya Kaskazini ‘B’, anasema baada ya kupata taarifa ya Muzne kukatishwa masomo, walifuatilia na kumrejesha shule.

Anaeleza kuwa taarifa za mtoto huyo kutoroshwa shule, walizipata kutoka kwa baba yake mzazi na kuanza kuchukua jukumu.

Ofisa Elimu Sekondari wilayani humo, Othman Khamis Machano, anasema baada ya shule kufunguliwa kutokana na corona mahudhurio ya wanafunzi si mazuri.

“Tulikaa pamoja na viongozi wa vijiji (masheha) kupita katika jamii kuhakikisha watoto wanakwenda shule kupata haki yao ya msingi,” anasema na kuongeza kuwa juhudi hizo ziliwarejesha wanafunzi shuleni na kwa sasa wanaendelea na masomo yao.

“Watoto walijenga hofu baada ya kujua athari za corona hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya majengo ya shule yalitumika kama vituo kwa ajili ya wagonjwa wa corona,” anasema Machano. Ofisa Elimu anaeleza kuwa wanaendelea kuwasisitiza walimu kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Juma Makame Haji, Msaidizi Mkurugenzi Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini ‘B’ Unguja, anawataka wazazi na walezi kuwa na ushirikiano na walimu wa shule ili kujua mahudhurio ya watoto wao.

“Mtoto Muzne alikatishwa masomo ya shuleni na madrasa lakini kwa sasa tunashukuru anaendelea na masomo yake,” anasema Machano.

**MTOTO ALITOROSHWA**

Mlezi wa Muzne ambaye ni shangazi yake, Mwajuma Hassan, anasema kipindi cha shule kufungwa kutokana na corona, mtoto huyo alichukuliwa na mama yake bila kumshirikisha ingawa ndiye anayemlea tangu akiwa mdogo.

Anasema wakati alipokwenda kumchukua binti yake, mlezi huyo alikuwa shambani wala hakufahamishwa lakini hata baada ya shule kufunguliwa mama yake aliendelea kumzuia, ili aendelee kulea wadogo zake.

“Baada ya kukaa huko muda mrefu akipitwa na masomo shuleni tuliamua kutoa taarifa serikalini ili kupata msaada. Nimeanza kumlea Muzne tangu akiwa na miaka mitatu na wala hana tabia ya utoro shuleni na ana fahamu vizuri masomo yake,” anasema shangazi mlezi.

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

# Wilaya inavyopigana kumaliza kero sugu ya madarasa mwakani



Mbunge wa Nachingwea, Dk. Amandus Chinguile (kulia), akikabidhi moja ya mifuko kati ya 1,800 ya saruji kwa wakuu wa shule na madiwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

WANAFUNZI 4,417 watahitimu elimu ya msingi katika Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi mwaka huu, huku makisio ya wale watakaochaguliwa kuingia kidato cha kwanza 2022 yakiwa ni asilimia 97.

Ili wanafunzi wote wanaosoma ambao wanatarajiwa kuchaguliwa kuingia kidato cha kwanza waanze masomo kwa pamoja, mikakati ya kumaliza uhaba wa madarasa katika shule zote za sekondari za wilaya hiyo inaanza.

Katika mazungumzo na gazeti hili, Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Nachingwea, Andrew Muhulo, anataja baadhi ya mikakati iliyojiwekea akisema wilaya ina shule 27 za sekondari, lakini 16 kati ya hizo zina uhaba wa madarasa 22 ambayo wanaendelea kuyajenga ili yakamilike mapema.

Anasema, ili kukamilika kwa madarasa hayo, inahitajika mifuko 3,320 ya saruji na tayari 1,800 kutoka kwa Mbuge wa Nachingwea, Dk. Amandus Chinguule, imeshapatikana na kwamba uhamasishaji unaendelea ili kupatikana sementi na vifaa zaidi.

Shule hizo ni za umma, hivyo wameamua kuishirikisha jamii na Nachingwea katika jambo hilo ili kila mmoja aone anachangia nini, kwenye ujenzi wa madarasa.

Anafafanua kuwa viongozi wa vitongoji, vijiji na kata wanahamasisha wananchi katika maeneo yao ili kujiwekea mikakati ya kuhakikisha uhaba wa madarasa katika sekondari za Nachingwea unamalizika.

Ofisa elimu huyo anaamini kuwa jitihada hizo wanafunzi wataweza kuanza masomo ya sekondari kwa pamoja na si kwa mafungu, kwa kuwa juhudi zinafanyika kumaliza kero ya uhaba wa madarasa.

"Bahati ni kwamba, wananchi wanatambua kuwa shule za umma ni mali yao, hivyo tunawashirikisha katika ujenzi ili kila mmoja aone anachangia nini, kwa ajili ya kumaliza kero hii ya kila mwaka," anasema.

Mkazi wa Mjini Nachingwea Simon Milanzi anasema, kwenye eneo lao wamekubaliana kuchangia Sh. 1,000 kila mtu na kutoa nguvukazi yao kusomba maji na mchanga kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mapya.

"Wananchi wamehamasika baada ya wadau wa elimu kufanya ziara za mara kwa mara kuhamasisha ujenzi wa miundombinu ya shule na hasa madarasa ili kuinua kiwango cha elimu," anasema Milanzi.

ATHARI ZA UHABA

Ofisa elimu huyo anasema, utaratibu wa wanafunzi kuanza masomo kwa mafungu kutokana na uhaba wa madarasa, unasababisha baadhi yao kubaki nyuma huku wengine wakipiga hatua kimasomo.

"Lengo la serikali ni wanafunzi wote wanaanza masomo kwa pamoja, kwani wakipishana baadhi yao watashindwa kufanya vizuri na hivyo kubaki nyuma kimasomo," anasema.

Anasema, uwepo wa madarasa ya kutosha, unasaidia kupunguza mrundikano wa wanafunzi, na kwamba mazingira kama hayo si rafiki kwa mwanafunzi katika kujifunza na hata pia kufundishiwa.

"Sisi huku kwetu tunataka hali hiyo iwe tofauti ili wanafunzi waanze kwa pamoja, lakini bila kuwapo kwa mrundikano, ambao kimsingi ni kero kwa wanafunzi na walimu wao," anasema.

Kwa mujibu wa maelezo yake hali hiyo inasababisha serikali kutoa maelekezo kila mwaka ya kujenga madarasa na kutaka yakamilishwe kwa wakati ili wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza waanze masomo pamoja.

Mbunge Dk. Chinguile anasema, ametumia zaidi ya Sh. milioni 22 za Mfuko wa Jimbo, kununua mifuko 1,800 ya saruji, na kwamba hiyo ni awamu ya kwanza ya ugawaji wa saruji kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule za sekondari jimboni mwake, na zitaendelea kutumiwa kuchangia zaidi.

"Ni wajibu wetu viongozi na wadau mbalimbali kushirikiana kuinua elimu wilayani kwetu kwa kuboresha miundombinu ikiwamo ujenzi wa madarasa," anasema Dk. Chinguile na kuongeza kuwa ni jukumu la kila mdau kuendelea kuchangia chochote ili kusaidia kukabiliana na kero kwenye sekta ya elimu, ziweze kumalizika hasa za uhaba wa madarasa ili wanafunzi wawe wanaanza masomo kwa pamoja.

"Bado kuna mahitaji makubwa ya madarasa na hata madawati kwenye shule mbalimbali za Nachingwea, hivyo wadau tuendelee kushirikiana kwa hali na mali," anasema.

Anasema, kama mbunge wa jimbo, ana wajibu wa kuhakikisha wanafunzi wanasomea katika mazingira rafiki kwa kuwaboreshea miundombinu ikiwamo ujenzi wa madarasa bora.

> "Sisi huku kwetu tunataka hali hiyo iwe tofauti ili wanafunzi waanze kwa pamoja, lakini bila kuwapo kwa mrundikano, ambao kimsingi ni kero kwa wanafunzi na walimu wao," anasema.

> "Ni wajibu wetu viongozi na wadau mbalimbali kushirikiana kuinua elimu wilayani kwetu kwa kuboresha miundombinu ikiwamo ujenzi wa madarasa," anasema Dk. Chinguile na kuongeza kuwa ni jukumu la kila mdau kuendelea kuchangia chochote ili kusaidia kukabiliana na kero kwenye sekta ya elimu, ziweze kumalizika hasa za uhaba wa madarasa ili wanafunzi wawe wanaanza masomo kwa pamoja.

ELIMU

NA ALLAN ISACK, ARUSHA

# WAKUU WA SHULE WANAPOLALAMIKIA

## • Ruzuku elimu bure kiduchu hainunui hata 'rimu'

WAKUU wa shule za msingi na sekondari za serikali katika halmashauri za Karatu na Arumeru mkoani Arusha, wamefunguka kuwa ruzuku ya elimu bure ya takribani shilingi 500 kwa mwezi kwa mwanafunzi ni kiduchu, kiasi kwamba haitoshelezi kuendesha shughuli za shule hizo.

Wanasema hayo wakati wa uchunguzi uliofanywa na Nipashe , Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Arusha (APC) na Shirika la Kimataifa linalosaidia vyombo vya habari la Internews kwenye shule 20, 10 za msingi na 10 za sekondari (majina yanahifadhiwa) mkoani humo.

Mmoja wa walimu wa shule ya msingi wilayani Karatu (jina tunalo), anasema fedha za ruzuku zinazotolewa ni kati ya Sh. 300 mpaka 500 kwa kila mwanafunzi kwa mwezi, kiasi kisichotosha kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

"Shule yangu inapokea ruzuku ya Sh. 272,000 kwa mwezi kwa ajili ya elimu bure kiasi cha fedha hizi zinagawanywa kwa wanafunzi 708, hivyo ukigawanya fedha hizi utagundua kila mtoto analetewa Sh.384 ni hela kidogo mno ukilinganisha na mahitaji ya shule na ya mwanafunzi," anasema.

Anaongeza: "Sera ya elimu bure imeelekeza kuwa fedha hizo, zitumie katika matumizi ya ukarabati wa miundombinu ya shule, kununua vifaa vya kufundishia kwa walimu na vya kujifunzia kwa wanafunzi, vifaa vya michezo na kulipa mishahara ya watumishi ambao siyo waajiriwa."



Wanafunzi shuleni wakiendelea na masomo darasani. **PICHA: ALLAN ISACK**

**LAZIMA KUJIONGEZA**

Mwalimu huyo anasema wanalazimika kujiongeza, ili kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za shule kutokana na ufinyu wa bajeti ya elimu bure. Anasema mbinu wanazotumia ni pamoja na kutumia fedha za madaraka zinazotolewa na serikali kwa walimu wakuu, kukopa na kuwachangisha wananchi kwa ajili ya kuendeleza shughuli za shule.

Mmoja wa wakuu wa shule za sekondari katika wilaya hiyo anadokeza kuwa shule yake inapokea fedha za ruzuku ya elimu bure kiasi cha Sh.4,618,357.97 kwa wanafunzi 445 kwa mwaka.

Kwa upande wa Arumeru mmoja wa wakuu hao anasema shule yake ina jumla ya wanafunzi 619 na wanapokea ruzuku ya Sh.400,000 kwa mwezi ikiwamo posho ya mwalimu mkuu ya Sh.200,000 na fedha nyingine zilizobaki zinatumika kwenye ukarabati wa miundombinu ya shule na maandalizi ya mitihani.

Anafafanua kuwa japokuwa serikali inatoa fedha hizo, bado shule inakabiliwa na matatizo mengi kama uhaba wa madarasa, vitabu, zina mazingira duni, ubovu wa vyoo, ukosefu wa chakula na mabweni lakini pia mimba za utotoni kwa baadhi ya wasichana hata kushindwa kumaliza masomo.

Mwalimu mwingine anaongeza: Sekondari yangu ina wanafunzi 1,270 na walimu 52 wanaopokea ruzuku ya Sh. milioni 2.7 kwa ajili ya fidia ya ada, kununua vifaa vya maabara za sayansi na kufanya ukarabati."

Kwa ujumla uchunguzi katika shule hizo, unabaini kuwa zinakabiliwa na tatizo la uchakavu wa miundombinu kama madarasa na majengo ya utawala, hazina maabara na vifaa kwa ajili ya wanafunzi wanaosoma sayansi.

**WAZAZI KUCHANGIA**

Licha ya serikali kutoa fedha za ruzuku kwa ajili ya elimu bure, bado wazazi na walezi huchangishwa michango mbalimbali kwa kuwa ruzuku haitoshelezi.

Olive Kisanga, mkazi wa kata ya Ganako, wilayani Karatu anasema ana watoto wanne, wawili wanasoma shule ya msingi na wengine wawili sekondari na kwamba amekuwa akichangishwa michango mbalimbali

"Mwalimu mwingine anaongeza: Sekondari yangu ina wanafunzi 1,270 na walimu 52 wanaopokea ruzuku ya Sh. milioni 2.7 kwa ajili ya fidia ya ada, kununua vifaa vya maabara za sayansi na kufanya ukarabati."

ikiwamo kulipa maji, michango ya chakula, mlinzi na fedha za kununua karatasi za mitihani ya majaribio. Hivi karibuni wakati wa kuwasilishwa kwa bajeti ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Mbunge wa Nkasi Kaskazini Aida Kenani, anasema bungeni kuwa michango inaendelea ila kwa kibali maalumu cha kuidai.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema serikali inatoa elimu bila ada na siyo elimu bure.

Aidha, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, anaongeza kuwa waraka wa serikali namba tatu wa mwaka 2016, ulieleza ushirikishwaji wa wazazi katika maendeleo ya shule, lakini shule hairuhusiwi kufukuza watoto kwa sababu ya michango.

Kwa mujibu wa waraka huo kuhusu utekelezaji wa elimu msingi bila malipo, serikali kupitia waraka namba tano wa mwaka 2014 kutoa elimu msingi (kuanzia awali hadi kidato cha nne bila malipo, azma ya serikali ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 ambayo ina lengo la kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuanza elimu ya msingi wanasoma bila kikwazo chochote iwe ada au mahitaji mengine.

Katika utekelezaji elimu bila malipo nyaraka na miongozo kadhaa ilitolewa ukiwamo mwongozo wa matumizi ya fedha za ruzuku ya uendeshaji kwa shule za msingi za serikali kufuatia uamuzi wa serikali elimu bila malipo.

Waraka namba tano wa mwaka 2015, umeelekeza kuwa utoaji wa elimu ya msingi bila malipo mwanafunzi atasoma bila mzazi au mlezi kulipa ada wala michango ya fedha iliyokuwa ikitozwa shuleni kabla ya kutolewa waraka huo.

Pia waraka wa elimu namba nane wa mwaka 2011 umeelekeza utaratibu kuhusu michango mbalimbali wanayotakiwa kutoa wazazi au walezi kulingana na makubaliano kupitia kamati au bodi za shule.

ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Bajeti hii 'ilivyopitiwa' na masuala haya muhimu

SERIKALI imetangaza bajeti ya Sh. trilioni 36 itakayotumika kwa mwaka wa fedha unaoanza Julai mosi hadi Juni 30, 2022, lakini, inayoelekea kusahau suala la corona.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aliwasilisha makadiro ya mapato na matumizi ya serikali bungeni Alhamisi iliyopita, bila kuzungumzia namna taifa litakavyoratibu suala la COVID-19.

Kutokana na kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa Tanzania si kisiwa Wizara ya Fedha na Mipango, ilitarajiwa kuwa ingeeleza namna ambavyo taifa litakabiliana na corona, kwenye ngazi ya taifa, kanda na kimataifa.

Kama Rais alivyosema taifa si kisiwa ni lazima kukabiliana na ugonjwa huo ambao unavyoelekea unajitokea nchini kila mwisho wa mwaka kuanzia Desemba hadi Aprili kwa mwaka wa pili sasa. Hili lilijidhihirisha kuanzia mwaka 2020 wakati serikali ilipofunga taasisi za elimu kwa miezi mitatu kukabiliana na corona.

Licha ya kwamba serikali imeunda timu ya wataalamu kwa ajili ya kuishauri kuhusu COVID-19 bajeti imebaki kimya haijasema neno iwapo imetenga fedha kwa ajili ya kudhibiti na kukabiliana na ugonjwa huo ambao katika mataifa jirani kama Kenya, Uganda na baadhi ya nchi za Afrika hasa Afrika Kusini umeendelea kuwa tishio.

Baada ya serikali kupewa mapendekezo na timu ya wataalamu ilitegemewa bajeti ingetenga fedha kwa ajili ya kutekeleza baadhi ya mikakati hiyo kwa kuandaa mipango kazi na gharama zake, zinazoelezea ni kwa namna gani Tanzania itakabiliana na wimbi la tatu la corona kwa kuangalia kile taifa lilichojifunza baada ya kupitia awamu mbili za COVID-19, mwanzoni mwa 2020 na ya pili ya mwishoni mwa 2020 na mwanzoni mwa mwaka huu hadi Aprili 2021 na mapendekezo ya kitaalamu.

Pengine bajeti ingeeleza ni kitu gani kitafanyika na fedha zilizotengwa kwa sababu watu wanahitaji kukingwa, kutibiwa na kuziwezesha hospitali na maeneo yote ya kutoa huduma za afya kuwakinga wafanyakazi wake wakati wa kutoa huduma hizo.

Watanzania walitegemea serikali isingekaa kimya kwa sababu suala la COVID-19 ni la dunia, kwa hiyo linahusu biashara kati ya Tanzania na sehemu nyingine duniani, hivyo raia wanahitaji ulinzi na biashara pia kulindwa.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha bajeti ya serikali Alhamisi iliyopita, bungeni jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO.**

Katika awamu zote za kuzuka corona, Tanzania imekuwa ikipambana na vikwazo kutoka kwa majirani zake ikishutumiwa kuwa inasambaza ugonjwa kwa majirani.

Mathalani, kulikuwa na maneno baina ya Tanzania na Zambia kuhusu usafirishwaji wa shehena kwa vile Zambia ilifunga mpaka wake kujiepusha na corona iliyohofiwa ingeingia kupitia mpaka wa Tunduma na njia za panya.

Aidha, Kenya nayo ilikuwa na mikwaruzano na madereva wa Tanzania kuwa wanaingiza corona nchini humo na kuwapima huku kukiwa na malalamiko ambayo pengine majawabu yake yangetokana na mikakati ambayo ingeonekana kwenye bajeti ya 2021/22 kwa kurejea mapendekezo ya ripoti ya kamati ya corona.

> Dozi za chanjo za corona kwa kila mmoja anayetaka kuinga Maka ni pamoja na Pfizer, Astrazeneca, Moderna na Johnson & Johson's. Hata hivyo, chanjo zilizozalishwa India na China zilikuwa bado kuruhusiwa, hivyo suala la corona bado linaendelea kuwa na nafasi kwenye bajeti ya serikali.

**TAIFA HALIWEZI 'KUJIKAUSHA'**

Kwa upande mwingine huu ndiyo wakati wa Mahujaji kujitayarisha kwa ajili ya Ibada ya Hijja Maka, je, mahujaji wa Tanzania wanafanyaje kupata taarifa kamili za vipimo na chanjo hiyo? Ni kwa sababu mambo yalivyo, siyo muda wa kunyamaza. Ni vyema kushirikiana kwenye juhudi za kitaifa, kikanda na kimataifa kukabiliana na COVID-19.

Wakati bajeti hiyo inaanza kujadiliwa Dodoma sababu Saudi Arabia, imeshatangaza kuwa hakuna mahujaji watakaoruhusiwa kukanyaga ardhi yake kama hawana chanjo ya corona.

Kwa mujibu wa taarifa za Hijja zilizo kwenye mitandao kila anayetaka kuhiji mwaka huu ni lazima awe amechanja chanjo mara mbili na tena akiwa ametumia dawa zilizoidhinishwa na serikali ya Saudia.

Dozi za chanjo za corona kwa kila mmoja anayetaka kuinga Maka ni pamoja na Pfizer, Astrazeneca, Moderna na Johnson & Johson's. Hata hivyo, chanjo zilizozalishwa India na China zilikuwa bado kuruhusiwa, hivyo suala la corona bado linaendelea kuwa na nafasi kwenye bajeti ya serikali.

**CHANJO/UTAFITI**

Watanzania wanataka pia kufahamu kupitia bajeti iwapo dawa ya mitidawa iliyoagizwa kutoka Madagascar imekuwa na tija kwa kupambana na virusi vya corona na kipi kinachoendelea baada ya ujio wa dawa hiyo ambayo mwaka jana serikali ilituma ndege kuichukua Antananarivo.

Wakati wa kuwasilisha bajeti, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki za Kenya na Uganda zilitaja mikakati na mafungu yaliyotengwa kwa ajili ya kununua chanjo, kuhamasisha jamii kujikinga na corona na mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya kukabiliana na maradhi hayo.

**DIASPORA KUPOROMOKA**

'Diaspora' kati ya mijini na vijijini imetikisika kutokana na kuwapo kodi ya muamala kuanzia Shilingi 10 hadi 10,000 inayotumwa na kupokea pesa kutegemeana na kiwango kinachotumwa na kupokelewa.

Kwa ujumla kutoza kodi hiyo kunaweza kukawakimbiza watumiaji waliowezesha kuviunganisha vijiji na miji midogo pamoja na majiji kupitia kutuma pesa zilizofanikisha mambo mengi vijijini.

Ni ukweli kuwa walioko mijini wanatuma pesa kufanikisha utatuzi wa masuala ya dharura kwa ndugu zao vijijini ikiwa ni pamoja na gharama za matibabu, uzalishaji mfano kwenye kilimo kununua mbegu, pembejeo, ufugaji na baishara mbalimbali na yote hayo yalifanikisha kuboresha na kuinua maendeleo vijijini.

Licha ya kwamba Waziri wa Fedha, anasema kodi ya muamala utakusanya Sh. bilioni 1.3 kuna uwezekano kuwa huenda ule uhusiano wa 'kidiaspora' uliowezesha miji na majiji kutuma fedha vijijini kuporomoka.

Aidha, suala la laini za simu nazo kuwa na kodi huenda likatikisa hatima ya diaspora hiyo iliyokuwa njia mojawapo ya kufanikisha maendeleo kwenye maeneo mengi nchini. Bunge lisaidie wananchi kutupia jicho eneo hilo.





# ‘Watendaji sababu Chemba kupata hati zenye shaka’

**Na Renatha Msungu,** CHEMBA

WATENDAJI wa Halmashauri ya Chemba, wametajwa kuwa chanzo cha halmashauri hiyo kupata hati yenye shaka, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo baadhi kutopeleka benki fedha zilizokusanywa.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Said Sambala, alitoa kauli hiyo katika kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo cha kujadili hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema pia kuwapo na upungufu katika ufungaji wa mahesabu huku baadhi ya nyaraka kutoonekana.

“Halmashauri kupata hati yenye shaka maana yake ni kwamba kuna baadhi ya watendaji hawatimizi wajibu wao kwa kuwa hali hii imekuwa ikijitokeza kila ikitoka ripoti ya CAG, hivyo kuna watu wanatakiwa kuwajibishwa,” alisema.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Abdi Msuri, aliwataka watendaji wote waliopewa dhamana ya kukusanya mapato ya ndani ya halmashauri kutekeleza wajibu wao kwa kuzingatia sheria, uaminifu na uadilifu.

Aliwaonya kuwa watakaokwenda kinyume wataondolewa katika nafasi hizo.

“Tumeomba sana tuwe pamoja lakini kama vile hatuendi kawaida, wakuu wetu hawana itifaki kabisa sasa itabidi tuchukuliane hatua hatutakuonea ila tutakutendea haki, ni uzembe ni uzembe ni uzembe, tuende kama timu kila mmoja awajibike mnasema eti wale ni wanasiasa iko siku utaona madhara ya hao wanasiasa,” alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Chacha, alisema kila mwaka kuna mapungufu katika ufungaji wa mahesabu na huo ni uzembe.

Alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Semistatus Mashimba, kuwasimamia watendaji wote na kuhakikisha kila mmoja anatimiza wajibu wake.

Dk. Mashimba alisema awali walikuwa wakikabiliwa na uhaba wa watendaji lakini kwa sasa limetatuliwa.

“Ole wako ukae na hela ya serikali nyumbani kwako tunataka upeleke benki mambo mengine yote tutayaweka vizuri tayari tumepata watu wenye weledi,” alisema.

**“Halmashauri kupata hati yenye shaka maana yake ni kwamba kuna baadhi ya watendaji hawatimizi wajibu wao kwa kuwa hali hii imekuwa ikijitokeza kila ikitoka ripoti ya CAG, hivyo kuna watu wanatakiwa kuwajibishwa,” alisema.**

# Tril. 12/- zilivyookolewa kesi dhidi ya serikali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndani ya miaka mitatu imeokoa zaidi ya Sh. trilioni 12 katika mashauri ya madai yaliyokuwa yamefunguliwa dhidi ya serikali.

Wakili Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, aliyabainisha hayo jijini hapa katika mafunzo ya mawakili wa serikali ya kuwaongezea uwezo kwenye uendeshaji wa mashauri.

Alisema ofisi hiyo ilianza kutekeleza majukumu yake mwaka 2018 na kwa kipindi hicho mafanikio mbalimbali yamepatikana ambapo kwa mwaka wa fedha 2019/20 ofisi hiyo ilifanikiwa kuokoa fedha ambazo zinatokana na mashauri yaliyofunguliwa dhidi ya serikali na taasisi zake Sh. trilioni 11.4

“Mwaka huo pia ofisi iliendesha mashauri mbalimbali ambayo hayahusishi fedha na kurejesha mali mbalimbali ikiwamo mashamba 106,” alisema.

Aidha, alisema kwa mwaka 2020/21, ofisi katika mashauri mbalimbali yakihusisha masuala ya kifedha iliokoa Sh. bilioni 643.7.

“Kama sio uimara wa Ofisi ya Wakili wa Serikali fedha hizo zingelipwa kwa watu wasiostahili na kuisababishia serikali hasara ya kiwango hicho,” alisema.

Pamoja na hayo, alisema ofisi hiyo imefungua ofisi zake kwenye Mahakama Kuu zote za Tanzania.

“Pia tumeanzisha mifumo ya TEHAMA ambayo inasomana na mahakama zote nchini katika kesi zilizofunguliwa zinazohusu serikali, tumeendesha mashauri mbalimbali nje ya nchi na ofisi hii ilipambana na kukomboa mali na kushinda mashauri husika ikiwamo ukamataji wa ndege Afrika Kusini,” alisema.

Hata hivyo, alisema pamoja na mafanikio hayo ofisi hiyo inakabiliwa na upungufu wa mawakili ambapo waliopo ni 88, huku mahitaji ni mawakili 308.

Malata akizungumzia kuhusu mafunzo hayo, alisema yatafanyika kwa siku nne ili kuwajengea uwezo mawakili wa serikali kwenye uendeshaji wa mashauri yanayofunguliwa dhidi ya serikali.

Akifungua kikao hicho, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, alisema mafunzo hayo ni muhimu kuwa endelevu kwa mawakili ili kuongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

“Mafunzo haya ni kwa ajili ya kuwaongezea ujuzi na weledi katika utekelezaji wa majukumu yenu na kuboresha mahusiano jambo ambalo ni muhimu katika utendaji kazi, mada muhimu zitagusiwa ikiwamo weledi katika uendeshaji wa mashauri ya madai,” alisema.

Prof. Kilangi alisisitiza mada hizo ni muhimu kwao katika uendeshaji wa mashauri ya serikali ndani na nje ya nchi.

“Lazima muwe na ujuzi wa kusimamia na kuendesha mashauri haya ndani na nje ya nchi inaweza kuwa kwenye Mahakama za Kimataifa au mabaraza ya kimataifa,” alisema.



Kiongozi wa Kanisa la Mlima wa Bwana Assemblies of God, Sabasaba jijini Dodoma, Askofu Sylvania Komba akiwa na waumini wake kuchangia damu, kanisani hapo juzi ili kuwasaidia wahitaji. PICHA: PETER MKWAVILA

# Mambo ya Ndani yazipa angalizo jumuiya

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema itazichukulia hatua kali jumuiya zote zilizopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambazo zitakiuka sheria na taratibu katika kujiendesha.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa Shirikisho la Wamiliki na Mameneja wa Shule na Vyuo binafsi (TAMONGSCO), jijini hapa.

Simbachawene alisema kuna watu ambao wamekuwa na utaratibu wa kuleta vurugu na kuzivuruga jumuiya hivyo wizara yake haitasita kuwachukulia hatua.

“Hata pingu ikibidi zitatembea kwa wahalifu, haiwezekani mtu akawa anavunja sheria halafu anaangaliwa tu na mimi nitatuma vyombo vya kufanya uchunguzi na tutachukua hatua kali kwa sababu watakuwa wamekiuka sheria za nchi.”

“Nasema songeni mbele atakayeleta shida mimi ndio nitakayeshughulika naye na salamu hizi ziwafikie jumuiya hizi zinaundwa kwa mujibu wa sheria za nchi, haiwezekani watu wakawa wanafanya masihara katika hili, tutachukua hatua kali kwa wale ambao wanavuruga vuruga,” alisema.

Naye Mwenyekiti wa Shirikisho hilo, Alfred Luvanda, alimshukuru waziri kwa kusimamia zoezi la uchaguzi wa kuwapata viongozi wapya halali wa shirikisho hilo.

“Sasa tutakuwa na uhuru wa kufanya mambo yetu pamoja na kuzungumza na serikali namna gani tunaenda katika ubia wa uendeshaji shule pamoja na nchini,” alisema.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Shirikisho hilo, Youstor Mtungi, alisema wanakabiliwa na kero kwa baadhi ya wenye shule kuchukuliwa kama wafanyabiashara kwa kutozwa kodi nyingi wakati wao wapo kwenye lengo la kutoa huduma ya kumsaidia mtoto yeyote wa Mtanzania kupata elimu.





# Mbowe ataja wachawi CHADEMA

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), umedai kuwa chama hicho kimekuwa kikishindwa kukubalika kwa wananchi na wagombea wake kushindwa kwenye chaguzi mbalimbali kutokana na uzembe wa baadhi ya viongozi wake.

Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, aliyasema hayo jijini Mbeya wakati wa mkutano wa ndani wa wanachama wa chama hicho Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Nyasa), uliolenga kutoa elimu ya kuhusu mageuzi ya kidijitali.

Alisema mara nyingi wamekuwa wakishindwa kwenye chaguzi wanasingizia kwamba Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho ni chama tawala kiliiba kura na baadhi wakidai kuonewa na serikali, lakini ukweli ni kwamba katika baadhi ya maeneo sio kweli.

Alisema baadhi ya viongozi wa chama hicho wamekuwa wakifanya kazi kwa maslahi yao binafsi, lakini kazi za chama hawashiriki, hali ambayo inakifanya chama hicho kukosa nguvu katika maeneo husika.

"Nataka tuachane na kila makosa yetu tunayasukumia CCM, utasikia mtu anasema CCM waliiba kura, CCM waliiba uchaguzi. Ni kweli wanaiba, lakini kuna maeneo kadha wa kadha ambayo tunashindwa kwa sababu ya uzembe na uvivu wetu wenyewe," alisema Mbowe.

Alisema ili chama hicho kifanikiwe kukiondoa CCM madarakani, ni lazima kijisahihihishe kwenye maeneo yote ambayo kilikuwa kinafanya makosa ikiwamo kufanya kazi ya kutafuta wanachama usiku na mchana.

Alisema kwa sasa baada ya kuanzisha mfumo wa kidijitali wa kusajili wanachama, chama hicho kitafika kwenye uchaguzi mkuu ujao kikiwa kinajitegemea kiuchumi bila kutegemea ruzuku ya serikali, na kwamba kazi ya kuing'oa serikali ya CCM madarakani itakuwa ya kudumu.

Aliwataka wanachama wa chama hicho kuanza maandalizi mapema ya kumpata mgombea wa nafasi ya urais na nafasi zingine mapema kabla ya mwaka wa uchaguzi, badala ya kuanza harakati za kuwapata wagombea miezi michache kabla ya uchaguzi.

**AMFAGILIA SAMIA**

Katika hatua nyingine, Mbowe alisema chama hicho kitaendelea kumpa ushirikiano Rais Samia Suluhu Hassan, kwa maelezo kuwa serikali yake inafanya kazi vizuri.

Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kupitia CHADEMA, Joseph Mbilinyi 'Sugu', alisema chama hicho bado kipo imara katika Jiji hilo, na kwamba wananchi wanakikubali kuliko hata ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Alisema Jimbo la Mbeya Mjini litaendelea kuwa ngome ya chama hicho pamoja na kwamba kwa sasa lipo chini ya CCM, na akawataka wanachama kuendelea kujiandikisha kwenye mfumo wa kidigitali.

Sugu alisema kwa sasa CHADEMA haiko tayari kupokea ruzuku ya serikali, kwa maelezo kuwa ni haramu badala yake wataendelea kutumia nguvu za wanachama kukiendesha chama.

"Kuna wale wenzetu ambao waliamua kuungana na serikali, wao wamepewa vyeo, lakini sisi tumebaki na heshima na hiyo heshima ndiyo silaha yetu kubwa," alisema Sugu.

Alimwomba Rais Samia kukutana na vyama vyote vya siasa kwa madai kuwa vyama hivyo ni miongoni mwa wadau muhimu wa maendeleo nchini.



Baadhi ya wajasiriamali wa soko la Kiwira katika Halmashauri ya Rungwe mkoani Mbeya, wakiwa wamelizunguka moja ya gari yanayopita katika eneo hilo kwa ajili ya kuuza matunda yao hasa ndizi. PICHA: NEBART MSOKWA

## Wauza mboga, serikali wapatana

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MGOGORO kati ya wafanyabiashara wa matunda na mboga wa Kiwira wilayani Rungwe na serikali umemalizika baada ya kukubali kutowaondoa wafanyabiashara hao kwenye eneo la hifadhi ya barabara mpaka watakapotafutiwa eneo mbadala.

Wajasiriamali hao walikuwa na mgogoro wa muda mrefu na Halmashauri ya Rungwe kutokana na kutakiwa kuondoa biashara kwenye eneo hilo kwa madai kuwa sio rasmi kwa kazi hiyo na ni hatari kwa maisha yao.

Wajasiriamali hao walikuwa wanagoma kuondoka wakidai kuwa hawana mahali kwa kwenda kufanyia biashara hizo wakidai kuwa eneo ambalo serikali ilikuwa inawapeleka ni mbali na barabara kuu na hakuna wateja.

Juzi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rungwe, Loema Peter, alikaa na wafanyabiashara hao na kukubaliana waendelee na biashara wakati serikali ikiendelea kuwatafutia eneo mbadala kwa ajili ya shughuli hizo.

Loema aliwataka wafanyabiashara hao kuwa makini wakati wanapoendelea na shughuli zao kwa maelezo kuwa katika eneo hilo wakati mwingine huwa kunakuwa na msongamano wa magari na hivyo kuwa na hatari ya kudhulika.

"Kwa sasa mtaendelea na biashara zenu na sisi tutaendelea kuwatafutia eneo ambalo mtakuwa salama na mtafanya biashara zenu kwa uhuru, lakini mwendelee kushiriki kwenye shughuli za maendeleo," alisema Loema.

Diwani wa Kata ya Kiwira, Michael Simon, aliishukuru serikali kwa kukubaliana na wananchi hao kwa maelezo kuwa walikuwa hawana amani na kulikuwa kunatokea vurugu mara kwa mara.

Aliwataka wafanyabiashara wawe huru na waendelee kufanya kazi zao wakati serikali ikiendelea na michakato mingine, na kwamba watapewa tena taarifa rasmi baada ya kupatiwa eneo mbadala.

Hata hivyo baada ya taarifa hiyo wajasiriamali wa eneo hilo waliibua shangwe wakidai kuachwa katika eneo hilo kutawasaidia kuendesha maisha yao vizuri.

# Bil. 40/- kupeleka umeme vijiji 114

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetenga zaidi ya Sh. bilioni 40.8 kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Umeme Vijijini (REA) awamu ya tatu katika Vijiji 114 vya Mkoa wa Mbeya, ambavyo vilikuwa havijaingia kwenye mradi huo.

Aidha imetenga Sh. bilioni 23.4 kwa ajili ya kujazilizia umeme kwenye vijiji ambavyo umeme wa REA awamu ya pili ulifika, lakini baadhi ya maeneo kwenye vijiji hivyo yalirukwa ama hayakuwa kwenye mpango.

Meneja wa Shirika la Umeme (TANESCO) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Fadhili Kalissa, aliyasema hayo jana alipokuwa anayatambulisha makampuni mawili ya makandarasi yaliyopewa tenda ya kusambaza umeme katika mkoa huo.

Kampuni zilizotambulishwa ni za kusambaza, kutawanya, kujenga na kuboresha miundombinu ya umeme (ETDCO) ambayo ni Kampuni Tanzu ya TANESCO iliyopewa kazi ya kusambaza umeme kwenye vijiji ambavyo havikufikiwa na REA na Kampuni ya Sagemcom Energy and Telecom LTD iliyopewa kazi ya kujaziliza umeme.

"Vijiji vitakavyonufaika ni 114 katika Mkoa mzima ambapo katika Wilaya ya Mbeya vipo vijiji 32, Chunya vijiji 12, Kyela vijiji 36 na Rungwe vijiji 34, lakini vijiji hivi ni miongoni mwa 150 ambavyo vilikuwa bado kufikiwa na huduma," alisema Kalissa.

Alisema kampuni hizo zimepewa muda wa miezi 18 kukamilisha miradi hiyo, na kwamba watahakikisha wanawasimamia makandarasi hao ili wakamilishe mradi ndani ya muda uliopangwa.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, aliwataka makandarasi waliopewa kazi hizo kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi na kwa wakati uliopangwa ili kuondoa malalamiko yasiyokuwa ya lazima.

Alisema ofisi yake itahakikisha inawapa ushirikiano makandarasi hao ili wakamilishe miradi hiyo kwa wakati nah ii ni utekelezaji wa maagizo ya rais kwamba viongozi tusimamie miradi.

"Kuna maeneo ambayo wananchi wanalalamika kwamba umeme umepita, lakini wao wamerukwa kwa hiyo hakikisheni malalamiko hayo mnayashughulikia pia," alisema Dk. Lutambi.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliiagiza Menejimeti ya TANESCO kuwasimamia kwa karibu makandarasi hao ili wakamilishe miradi hiyo kwa wakati uliopangwa kwenye mikataba yao.

Vilevile aliwataka maofisa habari na uhusiano wa shirika hilo kuainisha vijiji vyote ambavyo havijafikiwa na huduma hiyo na vipo kwenye miradi ili iwe rahisi kwa wakandarasi kuyaelewa na wananchi wajiandae.

Pia aliwataka makandarasi hao kushirikiana na taasisi zingine yakiwamo Magereza ili taasisi hizo pia zipate mapato kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao.

"Lakini mhakikishe mnashiriki kwenye shughuli za maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule, ujenzi wa zahanati na vituo vya afya, lakini hakikisheni umeme huo unazifikia taasisi zote za umma zikiwamo shule, ofisi za vijiji na vituo vya afya," aliagiza Homera.





## Rais Mwinyi afanya mazungumzo na Dk. Mpango

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi jana amekutana na kufanya mazungumzo na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango na kusisitiza haja ya kuendeleza ushirikiano kati ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Viongozi hao walifanya mazungumzo hayo Ikulu, jijini Zanzibar na mazungumzo kuhudhuriwa na baadhi ya viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Katika maelezo yake, Rais Dk. Mwinyi alimweleza Dk. Mpango kuwa anafarijika na juhudi kubwa zinazoendelea za ushirikiano uliopo wa Muungano na kila siku unazidi kuimarika.

Rais Dk. Mwinyi alisema kutokana na ushirikiano huo utasaidia changamoto zilizopo kushughulikiwa kwa haraka ili kuijenga nchi katika pande zote mbili za Muungano.

Akizungumzia suala zima la mazingira, Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa licha ya kuwa masuala ya mazingira si ya Muungano, lakini lina umuhimu wa kushughulikiwa katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema uharibifu wa mazingira si jambo la kubezwa hasa katika visiwa vya Unguja na Pemba, hivyo kuna kila sababu ya kuimarisha ushirikiano katika jambo hilo.

Pia pameweza kuwapo ushirikiano mzuri kati ya pande mbili hizo hata katika mambo yasiyohusiana na Muungano na hata kwa upande Wizara za Zanzibar zimepata fursa ya kujifunza mambo kadhaa kutoka katika upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye uzoefu mkubwa zaidi.

Rais Dk. Mwinyi alimpongeza kwa mara nyingine Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Mpango kwa nafasi aliyoshika huku akimpongeza kwa ziara yake anayoifanya ya kuitembelea Unguja na Pemba kwa mara ya kwanza tangu ashike wadhifa huo.

Naye Dk. Mpango alitoa shukurani kwa Rais wa Zanzibar pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kwa mapokezi mazuri aliyoyapata.

Alisema dhamira yake ya kuifanya Zanzibar kuwa ni sehemu yake ya kwanza ya kufanya ziara rasmi tangu ateuliwe kushika wadhifa huo na kueleza jinsi alivyofarijika na mwanzo huo mzuri.

Pia alimpongeza Rais Dk. Mwinyi pamoja na chama chake cha CCM, kwa kuchaguliwa kwa kishindo na wananchi wa Zanzibar.

Alisema hatua hiyo imetokana na wananchi kufurahi kwa kiasi kikubwa kuipokea Ilani ya CCM, pia wameridhishwa na dira yake wakati wa kampeni za uchaguzi ya kuiletea maendeleo Zanzibar.

# Serikali yaombwa kuongeza wahudumu wa sekta ya afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema kuwa wizara yake inatambua tatizo la wafanyakazi wa vituo vya afya hasa kisiwani Pemba.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Wawi, Bakar Hamad Bakar, aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kuongeza madaktari katika vituo vya afya kisiwani Pemba.

Waziri Mazrui alisema, tayari wizara yake imeomba serikalini jumla ya wafanyakazi 1,655, kati ya hao 519 Unguja na 1,136 Pemba wa kada mbalimbali za afya.

Alisema serikali itakaporidhia wafanyakazi hao watapangiwa kazi katika vituo vya afya vyenye mahitaji makubwa ikiwamo wilaya nzima ya mkoani Pemba.

Akizungumzia kuhusu bima ya afya, alisema kazi hiyo imeanza rasmi katika hatua ya awali na kamati ya kitaalamu ya kuanzisha mfuko wa bima ya afya inaendelea na kazi hiyo.

"Katika kukamilisha suala hili, kamati ya kuratibu masuala ya bima pia imeundwa ikijumuisha Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Ofisi ya Rais Katiba na Sheria na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar kwa lengo la kusimamia uanzishaji wa mfuko wa bima," alisema.

Alisema wizara anayoiongoza katika bajeti ya mwaka 2021/2022 imetenga Shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kununua vifaa tiba vitakavyotumika hospitali na vituo vyote vya afya.

Alisema utekelezaji wa ununuzi huo utategemea na hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Serikali Kuu.



Mkuu wa Kikosi cha Kuziwia Magendo Zanzibar, Azana Hassan Msingiri (kulia), akizungumza na wawekezaji kutoka kampuni ya Oilcom Ltd ya Dar es Salaam. Wengine ni Moh'd Mbaye ambaye ni kiongozi wa msafara wa kampuni hiyo (wapili kulia), Ali Haji Mmanga (katikati) na Kepteni Juma Ramadhani Juma. PICHA: RAHMA SULEIMAN

# KMKM yataja mikakati ya kuuza dawa hospitalini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) Commodore Azana Hassan Msingiri, amesema mipango ya kikosi hicho ni kuuza dawa kwa bei ya jumla katika hospitali zote za Zanzibar.

Hayo aliyasema jana huko makao makuu ya KMKM Kibweni, mjini Unguja, wakati akizungumza na mwekezaji kutoka kampuni ya Oil Com ya Dar es Salaam, Mohammed Mbaye, aliyefika na ujumbe wake kwa lengo la kuwekeza miradi mbalimbali katika kikosi hicho. Commodore Msingiri alisema tayari wamewasiliana na mwekezaji Mo Dewji ili awekeze katika hospitali hiyo, kutokana na kumiliki kiwanda cha dawa na lengo kuu la KMKM ni kujenga bohari kubwa kwa ajili ya kuhifadhia dawa hizo.

Naye Mbaye, alisema amefika katika kikosi hicho kuangalia maeneo ya kuwekeza miradi mbalimbali ambayo itafaa kutokana na eneo husika.

Alisema ni jambo la lazima kuunganisha nguvu pamoja na ujuzi ili kutomuangusha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, katika ahadi alizotoa ikiwamo suala la ajira 300,000 alizoahidi. Alisema ameamua kwenda kuwekeza katika kikosi hicho cha KMKM baada ya kuona ni sehemu sahihi ya kuwekeza na ina uwezo, nguvu kazi, ina heshima na ina maeneo makubwa kwa ajili ya uwekezaji wao na inastahiki kusaidiwa.

Alisema amevutiwa zaidi na maeneo waliyooneshwa ya Kibweni na Maisara ambayo yanafaa kwa uwekezaji wa aina yoyote.

Kwa upande wake, Kaimu Mkuu wa Utawala wa KMKM, Kamanda Juma Saleh Seif, amewapongeza wawekezaji hao kwa kukiamini kikosi hicho na kuona ndipo pahala sahihi kwa kuwekeza ndani ya kikosi hicho.

Alisema wawekezaji hao wamekuja wakati muafaka kwa kuwa kikosi hicho kimo katika mipango ya kuzalisha na tayari wamenunua boti kwa ajili ya uvuvi, pia ujenzi wa bekari kwa ajili ya uuzaji wa mikate ambao karibu utakamilika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NYUMBA YA GHOROFA INAUZWA**

**Ina frem za biashara, inafaa kwa makazi, au biashara kama Guest house au Hospitali. Ipo Ukonga Dar es salaam. Simu: 0757 079057.**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA MBEYA**
**SHAURI NO.11/2021**
**JOSEPH MWASIBUKA::::::::::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**SIMBINDA KASIMBILO:::::::::::::::::::MDAIWA**
**YAH : KUITWA SHAURINI**
**KWA :**
**SIMBINDA KASIMBILO**

Fahamu kwamba **JOSEPH MWASIBUKA** amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa **tarehe 24/06/2021** saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.A.Mapunda Mwenyekiti wa Baraza.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
**Kumbuka:** Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu NA lakiri/Muhuri wa baraza hili leo **tarehe 24/05/2021.**

**A.Mapunda**
**MWENYEKITI**
**24/05/2021**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 91 YA MWAKA 2020**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**PATRICIA FORTUNATA MWANUKUZI**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**MARGARET MALWA BANDORA & ANOTHER**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 29 Mwezi wa Juni, 2021.
Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 4 Mwezi wa Juni, 2021.

NAIBU MSAJILI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**
**WILAYA YA GEITA**

**MADAI NAMBARI 29/2021**

**MDAI…. EMILY NICOLAUS KAYANDA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA.HAPPINES EMMANUEL SIMON**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai ya **TALAKA**
Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya **tarehe 23/06/2021 saa 2:30 asubuhi** kwa kujibu madai hayo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo **tarehe 10/06/2021**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA RUNGWE**
**LILILOKO TUKUYU**
**KESI NA.42/2020**
**ALADIN MWANGOMO.......................................MDAI**
**DHIDI**
**ELIYAKIMU**
**MWAPALASYE.................................MDAIWA NA.1**
**ELIMA MWAIPOPO...........................MDAIWA NA.2**

**WITO/KUITWA SHAURINI**
**KWA**
**ELIMA MWAIPOPO**

Mdai aliyetajwa halo,amefungua kesi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Rungwe.Unaarifiwa kufika Baraza la Ardhi na Nyumba tarehe 21/06/2021 saa 2:30 asubuhi bila kukosa wewe au wakili wako au mtu yeyote utakayempa maelezo kamili.
Usipofika kama ulivyoamriwa,shauri hili litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.
AMRI hii imetolewa na mkono wangu na muhuri/lakiri ya baraza hili tarehe 24/05/2021.

**B.J.CYRIL**
**MWENYEKITI WA BARAZA**

---

**KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI**

DERICK NICHOLAUS MAKALWE ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SUNLG YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 917 AAX**. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KAH/ TR /RB/ 439/2019.**

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI/MAOMBI MADOGO/RUFAA NA. 232 MWAKA 2020**
**EZEKIEL S. KISOVU………**
**MUOMBAJI/MRUFANI**
**DHIDI YA**
**AZAPETRO D. MDEE NA WENZAKE….**
**…. MJIBU MAOMBI/MRUFANIWA**
**WITO/KUITWA SHAURINI**
**KWA AZAPETRO D. MDEE**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 29 Mwezi 6 Mwaka 2021 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mhe MBEGA mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamuriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Amri hii Imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/Muhuri wa Baraza hii leo tarehe 11 Mwezi 6 Mwaka 2021.

MWENYEKITI WA BARAZA

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI/MAOMBI MADOGO/RUFAA NA. 232 MWAKA 2020**
**EZEKIEL KISOVU………**
**MUOMBAJI/MRUFANI**
**DHIDI YA**
**AZAPETRO D. MDEE NA WENZAKE….**
**…. MJIBU MAOMBI/MRUFANIWA**
**WITO/KUITWA SHAURINI**
**KWA ROYAL RUNNERS**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 29 Mwezi 6 Mwaka 2021 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mhe MBEGA mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamuriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Amri hii Imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/Muhuri wa Baraza hii leo tarehe 11 Mwezi 6 Mwaka 2021.

MWENYEKITI WA BARAZA

---


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.181/2021**

Ombi la JULIUS WILLIAM MUHELO Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu DORICE JULIUS MUHELO
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 12/07/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 09/06/2021**

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

**KUPOTEA KWA CHETI**



**CHRISTIAN EDWIN MALUGU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1450/0028 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **EFATHA SEMINARY** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/DOD/RB/280252/2021.**

---

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie**
**0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Rais Edgar Lungu asema yu mzima baada ya kuzimia

**Lusaka,** ZAMBIA

RAIS wa Zambia, Edgar Lungu, amewahakikishia wananchi kwamba hana neno baada ya kuzimia akihudhuria mkutano wa hadhara.

Alikuwa akiongoza siku ya ulinzi hapo Jumapili wiki hii, mara ghafla akapoteza fahamu, akiwa mjini, Lusaka.

Katibu wa Baraza la Mawaziri, Simon Miti, alitoa taarifa akisema rais ni mzima na anaendelea na shughuli zake za kazi.

Dk. Miti alisema Rais Lungu alipata nafuu mara moja baada ya tukio hilo.

Rais alikabiliwa na hali kama hiyo ya kiafya mwaka 2015 na wakati huo ofisi yake ikisema kwamba ilitokana na tatizo katika umri wake.

Rais Lungu anagombea tena uongozi wa nchi hiyo katika uchaguzi mkuu utakaoandaliwa tarehe 12, mwezi Agosti, mwaka huu.

**BBC**

## Corona yaenea zaidi Uganda

**Kampala,** UGANDA

TAHARUKI imetanda Uganda wakati visa zaidi vya corona vikiendelea kuripotiwa kuenea kutoka sehemu mbalimbali za taifa hilo.

Aidha, familia kadhaa zimeshuhudia vifo vya jamaa zao baada ya kuugua ugonjwa huo wakakosa kupata matibabu stahiki kwa wakati.

Wizara ya Afya, ilisema watu 10,490 wamegunduliwa kuwa na virusi vya corona katika kipindi cha wiki moja tu huku 15 wakifariki kwa siku moja mwishoni wa wiki.

Zuio la kutovuka mipaka ya wilaya lilianza kutekelezwa kwa muda wa siku 42.

Kasi hiyo ya maambukizi ilileta wasiwasi kwenye vituo vya afya na vinaripoti kuzidiwa na wagonjwa wa Covid-19, vikipungukiwa, oksijeni.

Jeshi la Uganda limeingilia kati kuchangia katika kutengeneza gesi ya oksijeni ili kukabiliana na uhaba katika vituo vya afya.

Wakati huo huo, serikali ilitoa wito kwa yeyote aliye na ujuzi wa kutengeneza gesi hiyo avisaidie vituo vya afya ili kuokoa maisha.

Baadhi ya watu wana mtazamo kuwa kasi ya maambukizi inayoshuhudiwa kwa sasa imeongezeka kutokana na kupuuzwa kwa kanuni zilizowekwa.

Familia kadhaa zimeshuhudiwa zikitumia miti shamba pamoja na malimao, tangawizi na pilipili kujitibu au kujikinga.

**DW**

# Tshisekedi aahidi kujengea makazi waathirika volcano

**Goma,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi ameahidi kuharakishwa kwa ujenzi wa nyumba za muda kwa zaidi ya watu 15,000 ambao nyumba zao zimeharibiwa na volcano mjini Goma.

Amezuru mji huo, mwishomi mwa wiki, kwa mara ya kwanza na kuzungumza juu ya sababu za safari yake katika jiji hilo, liliiloathiriwa na mtiririko wa lava kufuatia mlipuko wa volkano Mei 22, mwaka huu katika mlima wa Nyiragongo.

Kiongozi huyo alitoa taarifa kuhusu mahitaji ya kibinadamu, pia usalama unahitajika katika eneo hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari, rais aliwahakikishia juu ya msaada utakaotolewa kwa waathiriwa wa volcano.

Alisema kuwa kuanzia Jumatatu wiki hii, atatembelea maeneo ambayo yametambuliwa katika suala hilo.

Alithibitisha azma ya serikali yake kuongeza kasi ya mchakato wa kupunguza Ziwa Kivu, ili kuepuka janga kubwa zaidi katika siku zijazo.

Pia alisema tafakari ni uwezekano wa kupanuliwa kwa jiji la Goma ambalo liko karibu kilomita 20, kutoka hatari volkano ya Nyiragongo.

"Lakini suala hilo halitafanyika kwa haraka na hakuna haki ya mtu itayopokonywa," alisema rais.

Kuhusu hali ya dharura iliyotangazwa huko Ituri na Kivu Kaskazini kwa zaidi ya mwezi mmoja, Rais Tshisekedi alisema atakagua maendeleo yaliyopatikana na udhaifu uliobaki.

Siku tatu kabla ya kuwasili kwa Tshisekedi, Goma, watu wasiopungua tisa, waliuawa na washukiwa wa wapiganaji wa ADF katika kijiji cha Mutuweyi-Mayamoto, mpakani kati ya majimbo ya Kivu Kaskazini na Ituri.

Katika ripoti yake, rais inaonyesha kusikitishwa na mashambulio hayo, pia anapongeza hatua chanya iliofikiwa na jeshi huku akiahidi kuendeleza shinikizo dhidi ya waasi.

"Hali ya dharura imeamuliwa kwa sababu wakati fulani ililazimika kutumia nguvu. Kikosi hiki kitatumika hadi kukabiliana na ngome ya mwisho ya wahalifu.

"Baada ya kutathmini hali hiyo, kutakuwa na mabadiliko. Ukweli ni kwamba katika safu ya vikosi vya jeshi la kitaifa kulikuwa na kasoro kadhaa, ninakusudia kufanyia kazi."

Wajumbe wa baraza lake la mawaziri walisema kwamba Rais wa Umoja wa Afrika (AU), Félix Tshisekedi alisema anaamini katika suluhisho la pamoja na za kikanda, kutatua kabisa shida za ukosefu wa usalama mashariki mwa nchi yake.

**RFI**



Naftali Bennett, Waziri Mkuu mpya Israel, akifurahia baada ya kupitishwa na bunge kushika nafasi hiyo, mwishoni mwa wiki, kuongoza serikali ya muungano baada ya uchaguzi wa mwaka jana. **PICHA: BBC**

# Isarel yapata Waziri Mkuu mpya baada ya Netanyahu

**Telaviv,** ISRAEL

NAFTALI Bennett atakuwa Waziri Mkuu mpya kwa miaka miwili kwa mujibu wa makubaliano yasiyo ya kawaida ya kushirikiana madaraka miongoni mwa vyama vinane vya kisiasa.

Vyama hivyo ni vyenye mtizamo mdogo wa pamoja ambavyo vililenga kumaliza uongozi wenye mzozo wa Benjamini Netanyahu.

Bennett ameapishwa jana kuwa Waziri Mkuu mpya wa Israel. Akiahidi kuliunganisha taifa hilo ambalo limeshuhudia uchaguzi mara nne ndani ya kipindi cha miaka miwili.

Alitoa kauli hiyo baada ya wabunge kupitisha kuundwa kwa serikali ya muungano kwa kupata ushindi mwembamba wa kura 60 kwa 59.

Serikali mpya ya Israel iliapishwa mwishoni mwa wiki na kumaliza utawala wa miaka 12 wa Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu na Bennett, mkuu wa chama kidogo cha kidini, kuchukua uongozi mpya wa taifa la wayahudi.

Bennett ni mshirika wa zamani wa Netanyahu ambaye alihudumu kama waziri wake wa ulinzi mwaka 2019 na mwaka jana.

Bennett mwenye umri wa miaka 49 baada ya miaka miwili, atamuachia uongozi Yair Lapid, mwenye miaka 57 ambaye aliwahi kuwa waziri wa fedha na mtangazaji wa zamani wa habari kwenye televisheni na ndiye aliyesimamia mpango wa kumuondoa Netanyahu.

Lapid alishinda kura ya pili kwa kishindo akiwa nyuma ya chama cha Netanyahu cha LIKUD, Machi mwaka huu, uchaguzi wa nne usiotoa maamuzi kwa Israel katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

**VOA/RFI**

# NEYMAR
## ATISHA BRAZIL IKIIUA VENEZUELA COPA AMERICA

**BRASILIA, Brazil**

KOCHA Mkuu wa Brazil, Tite amepaza sauti kumsifikia Neymar baada ya nyota huyo kuonyesha kiwango cha kuvutia wakati mabingwa watetezi hao wa Copa America wakianza michuano hiyo kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Venezuela, juzi Jumapili.

Neymar alifunga bao na kuhusika kwenye mabao mawili wakati Brazil wakiibuka na ushindi huo katika mchezo huo hapo Brasilia ambao ulichezwa huku mageti yakiwa yamefungwa na hakukuwa na mashabiki.

Marquinhos alianza kwa kufunga bao la ufunguzi baada ya kona ya Neymar dakika ya 23 kabla ya kupata penalti.

Lilikuwa bao la 67 la Neymar kimataifa akiwa amebakiwa na mabao 10 kuifikia rekodi ya ufungaji wa wakati wote kwa Brazil aliyoiweka Pele.

Tangu alipoanza kuichezea timu ya Taifa ya Brazil, Agosti 2010, mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain amefunga mabao 48 mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote wa sasa katika kikosi hicho cha Selecao.

Halafu Neymar akatengeneza krosi nzuri kwa Gabriel 'Gabigol' Barbosa aliyetokea benchi na kufunga bao la tatu dakika ya mwisho wa mchezo huo, na Tite akammwagia sifa, lakini akakataa kuwafananisha na magwiji wa Brazil, Ronaldo na Romario.

"Wakati Neymar akiwa fiti kiakili na kichwani kwake kuko poa, mambo mazuri yanatokea," alisema Tite akiwaambia waandishi wa habari kumsifia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29.

"Ukiwa na mchezaji ambaye ana ubora wa mbinu na mbunifu kama alivyo yeye, una nafasi kubwa ya kupata matokeo mazuri kwenye mchezo wowote uliopo mbele yako.

"Haitakuwa haki kulinganisha wachezaji kutoka zama tofauti, kwa sababu wachezaji wa kizazi changu walikuwa wa aina yake.

"Neymar pia ni wa aina yake, na muda uliopita Ronaldo na Romario pia walikuwa wachezaji wa aina yake."



## CALHANOGLU AWANIWA ATLETICO MADRID

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Atletico Madrid imeripotiwa kwamba, ipo tayari kumchukua kiungo wa AC Milan, Hakan Calhanoglu.

Nyota huyo wa kimataifa wa Uturuki, ambaye alicheza mechi waliyopewa kichapo cha mabao 3-0 na Italia Ijumaa kwenye Euro 2020, alikuwa na ushawishi mkubwa kuisaidia Milan kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa msimu wa 2020-21, huku akimaliza nafasi ya pili kwenye Serie A.

Calhanoglu alichangia pasi za mwisho 10 na mabao manne katika michezo 33 ya Serie A, lakini amechagua kutosaini mkataba mpya na Milan, na tayari walimpa mkataba mpya ambao aliukataa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anatajwa kuwa tayari kuondoka bure kabla ya msimu wa 2021-22 na ripoti za gazeti la Marca ni kwamba Atletico Madrid wamejitosa kuisaka saini yake.

Nyota huyo wa zamani wa Bayer Leverkusen, alipokea ofa kutoka Qatar na akafafanua kuwa yuko tayari kuhamia Galatasaray kabla ya mchezo wa ufunguzi kwenye mashindano ya Euro 2020.

Na sasa 'Los Rojiblancos' hao wameripotiwa kumpigania dhidi ya klabu kadhaa za Ulaya kuwania saini yake.

Klabu kadhaa za Ulaya zikiwapo za Ligi Kuu England, zimekuwa zikihusishwa na kuwania saini ya mchezaji huyo.

## ARSENAL WAPANGA KUIBOMOA LAZIO

**LONDON, England**

ARSENAL imewasilisha ofa ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Lazio, Joaquin Correa wakati huu wa usajili wa kipindi cha majira ya joto.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 raia wa Argentina, amefunga mabao 11 kwenye mechi 38 msimu uliopita, na bado ana mkataba wa kucheza hapo kwenye dimba la Olimpico.

Kwa mujibu wa ripoti nyingi nchini Italia, pamoja na Il Messaggero na La Repubblica, Biancocelesti timu hiyo imepokea ofa ya awali ya milioni 20 kutoka Arsenal, wakati 'Washikabunduki' hao wakiwa wanasaka mshambuliaji mpya kwa ajili ya msimu ujao.


Lakini taarifa nyingine zinaeleza kuwa, Everton pia wanavutiwa na huduma ya mshambuliaji i huyo ambaye thamani yake inatajwa kuwa Euro milioni 35.

Lakini, Il Messaggero wanaripoti kuwa kocha mpya wa Lazio, Maurizio Sarri, ameitaka klabu hiyo kutowauza wachezaji wao muhimu kwenye dirisha la uhamisho wa majira haya ya joto na Correa ni miongoni mwa wale ambao anataka kuwabakiza.

Correa ni zao la Academi ya River Plate, alijiunga na 'Biancocelesti' hao akitokea Sevilla kwa ada ya Euro milioni 15, mwaka 2018. Ana mabao mawili katika mechi tano na timu ya Taifa ya Argentina.

# BENZEMA FITI KUICHEZEA UFARANSA LEO

**PARIS, Ufaransa**



MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Karim Benzema, amewatoa wasiwasi mashabiki na kusema yupo fiti asilimia 100 kwa ajili ya mashindano ya Euro 2020, wakati kikosi chake kikitupa karata yake ya kwanza leo Jumanne dhidi ya Ujerumani.

Kocha Didier Deschamps alikanusha uwapo wa majeraha makubwa katika kikosi chake na Benzema sasa amebainisha kuwa tayari amerudi mazoezini kabla ya mchezo wa kwanza wa nchi yake kwenye mashindano hao leo.

"Najiskia vizuri sana. Nilianza tena mazoezi na timu jana," alisema mshambuliaji huyo wa Real Madrid akiiambia Telefoot.

"Hakukuwa na maumivu. Sikufikiria juu ya ukweli kwamba ningelazimika kupoteza Euro.

"Ilikuwa maumivu makubwa lakini ilikuwa pigo tu. Haikuwa lazima kukaa chini kwa muda sikutaka kijilazimisha, kwa hivyo niliamua kutoka.

"Tuna madaktari wazuri sana wa matibabu kwa hivyo kila kitu kilifanywa haraka sana. Ikiwa nilianza mazoezi tena na timu jana, ni kwa sababu sina usumbufu, sina maumivu.

"Ninajisikia vizuri, nilifanya kazi kwenye mazoezi kwa hivyo niko fiti asilimia 100."

# ERIKSEN

## AWATUMIA SALAMU WACHEZAJI WENZAKE

**COPENHAGEN, Denmark**

CHRISTIAN Eriksen anaendelea kupata ahueni hospitalini na ametuma salamu zake kwa wachezaji wenzake wa timu ya Taifa ya Denmark.

Eriksen alianguka muda mfupi kabla ya mapumziko katika mchezo wa ufunguzi wa michuano ya Euro 2020 ambapo Denmark ilikuwa ikichuana dhidi ya Finland Jumamosi usiku.

Mchezaji huyo wa Inter Milan mwenye umri wa miaka 29, alipata matibabu ya dharura uwanjani kabla ya kupelekwa hospitalini alikolazwa.

"Hali yake ni sawa na anaendelea kulazwa hospitalini kwa uchunguzi zaidi," ilisema taarifa ya Shirikisho la Soka Denmark.

"Leo asubuhi tumezungumza na Christian, ambaye ametuma salamu zake kwa wachezaji wenzake.

"Timu na wafanyakazi wa timu ya kitaifa wamepokea ushauri nasaha baada ya kushuhudia tukio hilo uwanjani na wataendelea kupeana motisha baada ya tukio la jana (juzi).

"Tungependa kumshukuru kila mtu kwa salamu zao za dhati."

Tukio la Jumamosi lilitokea wakati mpira ulipigwa kuelekea kwa Eriksen karibu na mwisho wa kipindi cha kwanza.

Wenzake waliofadhaika walimzunguka kumpa faragha japo katika hali ile mashabiki katika Uwanja wa Parken walionekana kukasirika wakati mchezaji huyo alipotibiwa.

Daktari wa timu ya Denmark, Martin Boesen, alisema Eriksen alikuwa amepoteza fahamu alipomfikia.

"Nilipomfikia alikuwa amelala upande, alikuwa akipumua, nilihisi mapigo ya moyo, lakini ghafla hilo ilibadilika," alisema.

"Msaada ulikuja haraka sana kutoka kwa timu ya matibabu na wafanyakazi wengine kwa ushirikiano wao, na tulifanya kile tulichopaswa kufanya na kufanikiwa kumrudisha Christian."

Mwezi uliopita, Eriksen aliisaidia Inter Milan kutwaa taji lao la kwanza la Italia kwa miaka 11 katika msimu wake wa kwanza kamili, baada ya kujiunga akitokea Tottenham Hotspur kwa pauni milioni 16.9 Januari 2020.

Eriksen alianza kama mchezaji wa timu ya vijana ya Ajax, kisha alihudumu kwa miaka saba akiwa na Tottenham, akiwafungia mabao 69 katika mechi 305 alizoshiriki.



# SOUTHGATE: STERLING KANIKUNA SANA

**LONDON, England**

GARETH Southgate amemsifia Raheem Sterling baada ya straika huyo wa Manchester City kufunga bao pekee wakati England ikiibuka na ushindi wa 1-0 kwenye mchezo wao wa ufunguzi wa Euro 2020 dhidi ya Croatia, Jumapili.

Sterling alitumia vizuri pasi ya Kalvin Phillips katika dakika ya 57 na kufunga bao hilo pekee kwenye mchezo huo wa Kundi D.

Kabla ya kuanza kwa mchezo huo, kulikuwa na mjadala mkubwa kwa mashabiki kama Sterling anatakiwa kuanza kikosi cha kwanza cha kocha Southgate au la kutokana na kuwa na msimu mbaya uliomalizika.

Pia alicheza mechi 12 zilizopita bila bao kwenye mashindano makubwa kwa kikosi hicho cha 'Simba Watatu'.

Baada ya kukosa nafasi nyingi za wazi kwenye mchezo huo, Sterling alisawazisha makosa yake na kufunga bao hilo muhimu lililowapa England pointi tatu.

"Nimefurahishwa na Raheem. Kwa muda mrefu kwenye michuano mikubwa hakufunga," alisema Southgate akiiambia BBC Sport.


"Nafikiri alikuwa hatari katika kipindi chote cha mchezo wa leo (juzi).

"Ni mchezaji mzuri na uwezo wake wa kufunga ni wa kuvutia, alipata nafasi nzuri na akafunga kwa kutumia ufundi mkubwa.

"Nafikiri bao lile limetupa hamasa kubwa kwenye mashindano haya, tuna wakati mwingine wa kupata mabao zaidi kwenye mechi zetu zijazo."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DE LIGT SASA AINGIA RADA ZA BARCELONA

●●●Miamba hiyo ya LaLiga tayari imewasajili Aguero na Eric Garcia, hivyo sasa inataka...

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA ina nia ya kumsajili mlinzi wa Juventus, Matthijs de Ligt, kwa mujibu wa Le10 Sport.

De Ligt alijiunga na Juve akitokea Ajax mwaka 2019, huku Cristisno Ronaldo akitajwa kuwa ndiye mshawishi wake mkuu baada ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya ulizikutanisha timu hizo mbili.

Lakini sasa, majaliwa ya De Ligt raia wa Uholanzi yapo kwenye mashaka na kwamba anataka kuondoka kwa 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin.

Barcelona walikuwa wakihusishwa sana na usajili wake kabla hajaondoka kwenye Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, lakini akatua Juve, na sasa miamba hao wa Catalunya wameingia tena kwenye mbio za kumuwania.

Miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, tayari wamewasajili wachezaji wawili kutoka Manchester City, Sergio Aguero na Eric Garcia.

Pia wanatajwa kwamba, wapo kwenye mbio za kuwania saini ya Memphis Depay kutoka Lyon na straika wa Borussia Dortmund, Erling Haaland.

Lakini sasa kwa mujibu wa ripoti ya Le10 Sport, Barcelona wanamtaka De Ligt kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ulinzi.

Inafahamika wazi kuwa kikosi cha Barcelona chini ya kocha Donald Koeman kinatarajiwa kujengwa upya ili kuwa na wakati mzuri kwa msimu ujao.

Hata hivyo, Barcelona wanaweza kukumbana na upinzani mkubwa kutoka kwa Manchester United ambao nao wanamwania.

## KWA UFUPI

**LEICESTER WAMTAKA COUTINHO**

KLABU ya Leicester City imepanga kumsajili kiungo wa Barcelona, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 29, ingawa bado haijapeleka ofa rasmi, klabu hiyo iko kwenye mazungumzo ya kumnasa Mbrazil huyo ikiwezekana kwa ada ya pauni milioni 17 au kwa mkopo. ***(Mundo Deportivo)***

**LEEDS YAMWANIA CORNET**

LEEDS United inamwania mlinzi wa kushoto wa Lyon, Maxwel Cornet mwenye umri wa miaka 24, lakini dau walilotajiwa la pauni milioni 20 kwa ajili ya kumnasa nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast, linawafanya kusita. ***(Sun)***

**ANCELOTTI AMTAKA WERNER**

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amewaarifu mabosi wa klabu hiyo kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Mjerumani Timo Werner mwenye umri wa miaka 25. ***(Fichajes, via Express)***

**MATA MSHAHARA KIDUCHU**

KIUNGO wa Hispania, Juan Mata mwenye umri wa miaka 33, atalazimika kuchukua mshahara wa pauni 70,000 kwa wiki kama anataka kuendelea kubaki Manchester United baada ya mkataba wake kumalizika mwishoni mwa mwezi huu. ***(Star)***

**ARTETA KUMUUZA LENO**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta yuko tayari kumuuza mlinda mlango wake, Bernd Leno mwenye umri wa miaka 29 raia wa Ujerumani, msimu huu kama atapatikana mbadala wake. ***(Mirror)***

**HAKIMI, EMERSON KUPISHANA**

CHELSEA imeongeza dau kwa ajili ya kumnasa mlinzi wa Inter Milan, raia wa Morocco Achraf Hakimi, ikiwamo kitita taslimu cha pauni milioni 43 pamoja na kumtoa nyota wa kimataifa wa Italia, Emerson Palmieri mwenye miaka 26. ***(Corriere dello Sport, via Express)***

**LEVY AFUNGUKA YA KANE**

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy amesema atafanya "kile kilicho sahihi kwa klabu" kuhusu masuala ya usajili, ikiwamo mustakabali wa mshambuliaji Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, aliyeonyesha nia ya kutimka msimu huu. ***(Goal)***

**ARSENAL YAMTAKA FEKIR**

ARSENAL wanamwania kiungo Mfaransa, Nabil Fekir kutoka Real Betis, lakini ofa ya 'Washikabunduki' hao haifikii kiwango kinachohitajiwa na klabu hiyo ya LaLiga kwa ajili ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(AS)***

**LIVERPOOL YAMWANIA ROMERO**

LIVERPOOL inaongoza kwenye mbio za kuwania saini ya beki wa Juventus, Cristian Romero raia wa Argentina, ambaye awali alihusishwa na mipango ya kutimkia Manchester United, baada ya kuonyesha kiwango kizuri akichezea Atalanta kwa mkopo. ***(Calciomercato - via Team Talk)***

**DE GEA HAJUI HATIMA YAKE**

GOLIKIPA wa Hispania, David de Gea mwenye umri wa miaka 30, inaelezwa kwamba hajui hatima yake ndani ya Manchester United wakati huu akijiandaa kufanya mazungumzo na kocha wa 'Mashetani Wekundu' hao, Ole Gunnar Solskjaer kuhusu mustakabali wake ndani ya Old Trafford. ***(Mirror)***

**ELIS AGOMBEWA EPL**

SOUTHAMPTON na West Ham ni klabu za hivi karibuni kutoka Ligi Kuu England, EPL, kuhusishwa na mipango ya kumsajili mshambuliaji wa Boavista, Alberth Elis mwenye umri wa miaka 25, huku Brighton na Watford awali zilionyesha pia nia yao ya kumnasa nyota huyo wa kimataifa wa Honduras. ***(A Bola)***

HABARI MICHEZO

# MSIMU AKIRI HAUKUWA MSIMU RAHISI KMKM UBINGWA Z'BAR

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM, Ame Msimu, amesema licha ya kufanikiwa kutimiza malengo yao hayo ya kubeba taji hilo msimu huu, haikuwa rahisi lakini hiyo sasa ni safari ya kuelekea kutimiza malengo yao ya muda mrefu ya kulibeba kwa misimu mitatu mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Msimu alisema lengo lake la kuchukua ubingwa huo msimu huu umekwenda sambamba na mipango ya timu hiyo kuhakikisha inakuwa timu kubwa na yenye wachezaji wenye uwezo katika Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema timu za Ligi Kuu Zanzibar msimu huu zilifanikiwa kusajili wachezaji wazuri na waliosumbua uwanjani hali iliyosababisha bingwa na hata zilizoshuka daraja kujulikana mwishoni mwa msimu.

"Tunashukuru tumekuwa mabingwa, lakini msimu huu ligi ilikuwa na upinzani mkubwa sana, kila timu ilikuwa ikitaka kujiweka sehemu nzuri isishuke na zile zenye nia ya ubingwa zilikuwa zikipambana," alisema.

Aidha, Msimu alisema mbali ya kunyakuwa ubingwa huo, lakini changamoto ya kutokuwa na udhamini kwenye Ligi Kuu Zanzibar, inaendelea kuzitesa klabu za ligi hiyo jambo ambalo linasababisha timu kushindwa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu kutoka nje ya Zanzibar.

"Tunasajili wachezaji wetu wengi wa ndani hapa Zanzibar kama ni nje basi ni kutoka Tanzania Bara, ni timu moja au mbili ndizo zimesajili wachezaji kutoka nje ya Tanzania, hii kidogo inasababisha hata wachezaji wetu kutopanda viwango vyao kwa sababu hawapati changamoto kutoka kwa wachezaji wa nje pengine," alisema.

Alisema timu za ligi hiyo zinakabiliwa na ukata mkubwa wa fedha na hata kushindwa kufanya maandalizi ya michezo yao mapema kuelekea msimu ujao kutokana na kutafuta kwanza pesa.

Hata hivyo, ameiomba serikali kutia mkono wake ili kulisaidia Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), katika suala la kutafuta wadhamini jambo ambalo litawapunguzia mzigo mkubwa viongozi klabu.

KITU HICHO...




Mshambuliaji na nahodha wa Taifa Stars, John Bocco, akijiandaa kuachia shuti lililojaa nyavuni na kuiandikia timu yake bao la kwanza wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Malawi kwenye mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Zitto ataka wachezaji kupewa uraia pacha

**Na Adam Fungamwango**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ameitaka serikali kufikiria kubadilisha sheria ya uhamiaji, ili kuruhusu uwapo wa wachezaji wenye uraia wa nchi mbili kwa ajili ya manufaa ya michezo Tanzania.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Zitto alisema hata kama serikali haitaki kufanya hivyo kwa raia wote, lakini iangalie suala hilo kwenye nyanja za michezo kwa sababu nchi inapoteza wanamichezo wengi ambao ni Watanzania wenye uraia wa nchi zingine na wenye vipaji, ambao wangeweza kulipatia sifa taifa pamoja na mapato pia.

"Mfano kuna mchezaji mmoja anaitwa Yusuph Poulsen, huyu baba yake ni Mtanzania kutoka Tanga, huko nyuma aliwahi kusema kuwa kabla ya kucheza timu ya Taifa ya Denmark alikuwa anataka kuchezea timu ya Tanzania, Taifa Stars, lakini ikashindikana kutokana na kutokuwapo kwa sheria hiyo," alisema kiongozi huyo.

Zitto alisema kwa sasa suala uraia pacha umekuwa ukizinufaisha sana nchi za Comoro, Madagascar na hata Cape Verde ambazo wachezaji wao wengi wamekuwa wakitoka nje ya nchi, lakini wenye asili ya nchi hizo na wamezibadilisha nchi hizo kutoka kuwa timu vibonde na sasa ni tishio kwenye soka la Afrika.

"Madagascar na Comoro wachezaji wao wana uraia wa nchi hiyo na Ufaransa, tena wanacheza kwenye klabu ndogo tu za madaraja ya chini, lakini wakija Afrika na kuchanyikana na wenzao wanakuwa tishio. Cape Verde pia, wachezaji wao wengi wana uraia pia wa Ureno. Nchi hiyo kwa kutumia wachezaji hao wamekuwa wanafanya vizuri sana," alisema.

Kiongozi huyo alisema Tanzania ina watu wengi ambao wametapakaa duniani na kuchukua uraia huko au wale waliozaliwa nje ya nchi lakini wazazi wao ni Watanzania, na wamekuwa wakitaka kuisaidia nchi yao ya asili, hasa kwa wanamichezo, lakini wamekuwa hawapati fursa hiyo.

## Kambi Taifa Riadha kuendelea - Serikali

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imesema kambi ya timu ya Taifa ya Riadha haitavunjwa hata baada ya wachezaji kwenda Japan kwenye michuano ya Olimpiki.

Timu ya Tanzania itaondoka Juni 29, kwenda Nagai, Japan ambako itapiga kambi kwa maandalizi ya mwisho kabla ya kwenda jijini Tokyo, kwa ajili ya michuano ya Olimpiki 2020 itakayoanza Julai 23 hadi Agosti 8, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Dk. Yusuph Singo, alisema hata baada ya timu hiyo kuondoka, kambi ya taifa iliyopo Arusha itaendelea kwa ajili ya maandalizi ya michezo ijayo ya Madola na ile ya Afrika.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akipokea msaada wa vyakula kwa timu hiyo uliotolewa na Kampuni ya Usafirishaji Mizigo ya China na Dubai ya Silent Ocean.

Vyakula vilivyokabidhiwa siku hiyo ni pamoja na unga wa ngano, unga wa sembe, mafuta ya kupikia na tambi, lakini na sabuni za kuogea na kufulia na dawa za meno.

"Wanariadha 20 wako kambini, watatu kati yao wamefuzu na watano tutawapeleka Nigeria ili kutafuta viwango kwenye mbio ndefu za uwanja (mita 5,000 na 10,000), tunawashukuru wenzetu wa Silent Ocean kwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kusaidia timu zetu," alisema Dk. Singo.

## Karia akunwa na vijana Stars

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, amesema mbali ya kufurahishwa na ushindi wa mabao 2-0, ambao timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, imeupata dhidi ya Malawi, lakini amefurahishwa zaidi kuona matunda ya yosso waliokwenda nchini Gabon kucheza Fainali za Afrika chini ya miaka 17, mwaka 2017 yameonekana.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Karia alisema kulikuwa na maneno huko nyuma kuhusu wachezaji wa timu ya Serengeti Boys waliocheza fainali hizo kuwa hawaonekani, lakini kwenye mechi hiyo dhidi ya Malawi wameonekana na kuonyesha viwango vya hali ya juu.

"Nawashukuru Malawi kwa kukubali kucheza na sisi kwenye tarehe za FIFA, niwashukuru wachezaji kwa kucheza vizuri na walistahili kushinda, mwalimu na benchi lake la ufundi. Nimefurahi kwa ushindi, lakini nimefurahi ile kauli ya watu wengi kuwa wale vijana wa Gabon hawaonekani, leo imefutika, tumewaona kama wanne wamecheza," alisema Karia.

# Michezo

Jumanne Juni 15, 2021

Nipashe




DE LIGT SASA AINGIA RADA ZA BARCELONA HABARI UK 22

HUPITI...



Mshambuliaji wa Brazil, Neymar akipiga hesabu za kumtoka straika wa Venezuela, Josef Alexander Martinez kwenye mechi ya michuano ya Copa America iliyopigwa Uwanja wa Nacional de Brasilia, Brazil juzi na wenyeji kushinda 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# UCHAGUZI TFF WABURUZANA FIFA

## ●●●Kidau aonya Tanzania kufungiwa, mgombea urais mwingine akimbilia wizarani huku...

**Na Saada Akida**

WAKATI wadau wa soka na Watanzania kwa ujumla, wakisikilizia mchujo wa wagombea wa nafasi mbalimbali kwenye Uchaguzi Mkuu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF) kwa waliorejesha fomu kwa Kamati ya Uchaguzi ya shirikisho hilo, wingu zito limetanda baada ya kuburuzana Shirikisho la Soka duniani, FIFA.

Hatua hiyo ya kuburuzana Fifa imekuja baada ya Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa TFF, Abdallah Bulembo, kuwasilisha barua ya malalamiko kwa shirikisho hilo la soka duniani, akipinga kitendo cha wachezaji wa zamani kunyimwa fursa ya kugombea nafasi kiti cha urais kwa kigezo cha kutokuwa na elimu ya chuo kikuu(shahada).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Bulembo, alisema sababu kubwa iliyomlazimu kutinga Fifa ni kipengele hicho kinachowanyima haki wachezaji waliocheza mpira kuwania nafasi ya urais kwa kigezo cha elimu ngazi ya shahada, lakini serikali kupitia wizara husika ya michezo nayo kukaa kimya bila jibu lolote baada ya kuwasilisha malalamiko hayo.

Bulembo alisema Mei 5, mwaka huu, aliwasilisha barua Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo akiwataarifu uchaguzi wa TFF unakaribia, hivyo kuna baadhi ya vipengele vya kanuni havitoi uhuru katika Katiba ya TFF na kuhitaji kufanyiwa marekebisho, lakini hakupata majibu yoyote.

"Hivyo, Juni 9, mwaka huu niliwasilisha barua FIFA nikiwaeleza Kanuni za TFF zinashida ndani ya katiba yake, bado sijapata jibu lolote ila nitajibiwa na pingine watakuja.

"Ninachozungumza isiwe ajenda kubwa kati yangu na Rais Wallace Karia (anayetetea kiti chake TFF), bali ni suala la wachezaji kutengwa na kanuni za wachezaji waliocheza soka kutopewa nafasi ya kugombea kwa sababu ya ukosefu wa shahada, mfano kwa Mbwana Samatta anayecheza soka Ulaya, endapo atarudi hataweza kugombea kutokana na kigezo hicho," alisema Bulembo.

Alisema kipengele kingine ni rais anayechaguliwa kumteua makamu wa rais ndiyo apigiwe kura, nacho kinapaswa kufanyiwa marekebisho na kuwa cha kuchaguliwa na wanachama kama ilivyokuwa awali na baadaye waende kwenye uchaguzi.

Naye mgombea anayewania nafasi ya urais, Ally Saleh 'Alberto', alisema amewaandikia barua wizara husika ya michezo na msajili wa vyama kushughulikia mapungufu yaliyomo kwenye Katiba na Kanuni za Uchaguzi za TFF.

"Hakuna chama chochote cha soka visiwani Zanzibar ambayo ni mwanachama wa TFF, hali ambayo inawanyima uhuru kugombea kwa kukosa wadhamini," alisema Saleh.

Wakati Bulembo na Saleh, wakieleza hayo, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidau, alisema mchakato wa uchaguzi ni mali ya Kamati ya Uchaguzi wa TFF kwa mujibu wa Katiba na Kanuni inayosimami vigezo hivyo na kwamba vimewekwa miaka miwili iliyopita huku kigezo cha elimu ya shahada kikiwa kimewekwa tangu mwaka 2006.

Kidau alisema mchakato wa uchanguzi huo uko chini ya Kamati ya Uchaguzi na watu wasiingilie kwa kutaka kupeleka mambo hayo nje ya mamlaka ambayo haihusiani na soka kuepuka madhara yakiwamo kufungiwa na Fifa.

"Kuhusu elimu tukumbuke miaka ya nyuma kulikuwa na fungiafungia nyingi hasa kulingana na viongozi kutokuwa na elimu na mchakato huo uliofanywa kuanzia 2006 ambapo kulikuwa na kipengele cha elimu.

"Hata kipengele cha wadhamini, viongozi wa TFF hawahusiki kabisa na suala hilo kwa sababu ni la mgombea na wanachama, kama shirikisho tuliwajulisha wanachama wetu kwamba mgombea urais anatakiwa wadhamini watano na mjumbe mdhamini mmoja," alisema Kidau.

Alisema wadau wanatakiwa kuheshimu mchakato huo kwa kuiachia Kamati ya Uchanguzi TFF na muhimu mpira uchezwe, wasikubali kuingia katika migogoro ambayo itawaweka katika wakati mgumu wa kufungiwa na kushindwa kushiriki michuano ya kimataifa kwa ndani ya taifa na klabu.

# YANGA YAZIPIGA BAO AZAM, SIMBA

**Na Saada Akida**

KLABU ya Yanga imefanikiwa kuwapiga bao la kisigino watani wao wa jadi, Simba na wapinzani wao wakuu, Azam FC kwenye mbio za kuinasa saini ya mshambuliaji wa Mbeya City, Denis Kibu kuelekea msimu ujao.

Taarifa za uhakika zilizofikia gazeti hili jana, nyota huyo aliyeonyesha kiwango cha juu msimu huu akiwa na Mbeya City na kisha kudhihirisha uwezo wake huo baada ya kuhusika katika mabao yote mawili wakati Taifa Stars ikishinda 2-0 dhidi ya Malawi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, alikuwa akiwaniwa na klabu hizo kubwa tatu nchini, lakini Yanga imefanikiwa kumaliza mchezo huo.

Mtoa habari huyo aliliambia Nipashe kuwa Yanga imekubaliana naye kusaini kwa dau la Sh. milioni 40 huku Azam FC wakiweka mezani milioni 30 wakati Simba hawakupata nafasi ya kuweka mzigo mezani baada ya kuelezwa ameshakubaliana na watani zao hao.

Nipashe lilipomtafuta, Kibu alikiri kufuatwa na timu zote tatu na kueleza anaangalia maslahi licha ya Yanga kuwa na nafasi kubwa kwa sababu walifanya naye mazungumzo juzi.

"Ni kweli klabu zote walinihitaji na kutaka huduma yangu, ikiwamo Simba, Azam FC na Yanga ambao nimefanya nao mazungumzo na nina imani kubwa kila kitu kitakuwa sawa," alisema Kibu.

Alipoulizwa Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa, alisema makosa ambayo walifanya kwenye usajili kipindi cha nyuma hayatajirudia na kwamba wanajipanga vizuri kwa kusajili kulingana na mahitaji ya timu yao.

"Safari hii tunaye kocha ndiye mwenye jukumu la usajili, tutasimama katika mapendekezo yake tofauti na msimu uliopita ambao tulisajili bila ya kuwapo kwa kocha mkuu, ila sasa tunaye Nabi [Nasreddine] na ametoa muongozo juu ya nafasi na aina ya wachezaji anaowahitaji," alisema.

Kwa upande wa Azam FC, Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema hawakuwa na mpango wa nyota huyo kwa sababu hakuwa katika mapendekezo ya benchi lao la ufundi linaloongozwa na kocha George Lwandamina.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002